# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Taarifa za Utafiti, Uchambuzi wa Mifumo na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Rasilimali za Umma katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**
**2018/2019**

**Imeandaliwa na :**
**Idara ya Uzuiaji Rushwa**
**Makao Makuu-Dodoma**
**Tanzania**

## DIBAJI

Jarida hili ni mkusanyiko wa baadhi ya kazi za uzuiaji rushwa zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa 2018/2019. Lengo la jarida ni kuufahamisha umma hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuzuia rushwa. Uandaaji wa jarida hili ni matokeo ya utekelezaji wa kifungu cha 7 (a) na (c) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba. 11 ya mwaka 2007, kinachoitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutath mini, kuchambua na kufuatilia utendaji kazi wa mifumo mbalimbali ya utoaji huduma kwa minajili ya kuainisha maeneo yenye udhaifu na mianya ya rushwa na kisha kuishauri namna bora ya kuiziba mianya hiyo na hivyo kuimarisha mifumo. Kazi za uzuiaji zilizomo kwenye andiko hili ni zile zilizohusisha uchambuzi wa mifumo, utafiti na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (fedha) katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo maji, elimu, afya, na ujenzi wa miundo mbinu. Kimuundo jarida limeandaliwa kulingana na utangulizi wa kazi iliyotekelezwa, matokeo, mapendekezo na mafanikio ya hatua ambazo Taasisi imezichukua.

Jarida hili ni muhimu kwa vile linaelimisha na kuongeza hamasa ya wananchi na wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kupambana na rushwa. Ni matumaini yetu kuwa matokeo yaliyomo kwenye jarida hili yatasaidia kuzifumbua macho taasisi/ofisi ambazo zimeguswa na kazi zetu za utafiti, uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji na hivyo kuziwezesha kuandaa mikakati ya kuzuia rushwa. Aidha, TAKUKURU inaamini kuwa mapendekezo yaliyomo kwenye jarida hili yakitekelezwa yatasaidia kuimarisha mifumo ya utoaji huduma na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi. Hii ni kwa sababu rushwa ni utawala bora ni maadui wasioweza kuishi pamoja. Tunatoa rai kwa umma wote wa watanzania kuunganisha nguvu zetu ili tuweze kushinda vita dhidi ya rushwa. Ukweli ni kwamba Serikali peke yake haiwezi kushinda vita hii bila nguvu ya wananchi.

Mwisho, tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwa taasisi/ofisi/vyama au watu binafsi ambao kwa namna moja au nyingine walijitoa na kuwa tayari kutoa ushirikiano pale tulipohitaji. Aidha, tunaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuwezesha na kufanikisha kutekeleza jukumu hili la msingi. Kipekee kabisa, tunampongeza Jemedari wetu Mkuu katika mapambano haya Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuonyesha njia kwa vitendo katika kuongoza mapambano dhidi ya rushwa nchini. Utashi aliounesha kisiasa ni ushahidi tosha kwamba anachukizwa na rushwa. Vilevile tunapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wadau wetu wa Maendeleo (DPs) kwa kutupatia fedha ambazo zimefanikisha utekelezaji wa jukumu hili. Wadau hao ni Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Tunapenda kuushukuru umma wa Watanzania kwa kuendelea kuonesha imani kwa chombo chao na kutuunga mkono katika vita hii ambayo ni lazima tuishinde kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................... i

YALIYOMO ........................................................................................................... iii

ORODHA YA VIFUPISHO ........................................................................................................... vii

1.0 MFUMO WA UKUSANYAJI MAPATO KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI ............... 1

1.1 Utangulizi ........................................................................................................... 1

1.2 Matokeo ya Uchambuzi ........................................................................................................... 2

1.3 Mapendekezo ........................................................................................................... 5

1.4 Mafanikio na Hitimisho ........................................................................................................... 7

2.0 MIANYA YA RUSHWA KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA USAFIRI WA UMMA JIJINI DAR ES SALAAM ........................................................................................................... 8

2.1 Utangulizi ........................................................................................................... 8

2.2 Matokeo ya Utafiti ........................................................................................................... 9

2.2.1 Kukinzana kwa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ukusanyaji wa Mapato ................. 9

2.2.2 Udhaifu katika Ukusanyaji wa Mapato Kituo cha Mabasi Ubungo ....................... 11

2.2.3 Ukiukwaji wa Mikataba ya Maegesho ya Magari ................................................ 12

2.2.4 Mianya ya Rushwa katika Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali .............................. 13

2.3 Mafanikio na Hitimisho ........................................................................................................... 16

3.0 RUSHWA KATIKA HUDUMA ZITOLEWAZO NA VYAMA VYA MSINGI VYA KILIMO NA MASOKO (AMCOS) VYA ZAO LA KOROSHO NCHINI ................................ 18

3.1 Utangulizi ........ 18
3.2 Matokeo ya Uchambuzi ........ 19
3.3 Mapendekezo ........ 20
3.4 Mafanikio na Hitimisho ........ 21
4.0 TATHMINI YA UFANISI WA MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI KATIKA KUONGEZA MAPATO YA SERIKALI (EFDs) ........ 22
4.1 Utangulizi ........ 22
4.2 Matokeo ya Utafiti ........ 23
4.2.1 Mitazamo ya Wafanyabiashara Kuhusu Matumizi ya Mashine za Kielekroniki ........ 23
4.2.2 Matokeo Yaliyopatikana Kutoka Uwandani (Practical Evidence) ........ 24
4.3 Mapendekezo ........ 26
4.4 Mafanikio na Hitimisho ........ 27
5.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI YA KITAIFA ........ 28
5.1 Utangulizi ........ 28
5.2 Matokeo ya Ufuatiliaji ........ 29
5.3 Mapendekezo ........ 30
5.4 Mafanikio na Hitimisho ........ 31
6.0 RUSHWA KATIKA MFUMO WA UHAULISHAJI AWAMU III WA TASAF ........ 32
6.1 Utangulizi ........ 32
6.2 Utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Tatu (TASAF III) ........ 33
6.3 Matokeo ya Ufuatiliaji ........ 33
6.4 Mapendekezo ........ 34

6.5 Mafanikio na Hitimisho ........ 34
7.0 RUSHWA KATIKA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA CHAMA CHA USHIRIKA CHA KINYAKI ........ 36
7.1 Utangulizi ........ 36
7.2 Matokeo ya Ufuatiliaji ........ 37
7.3 Mapendekezo ........ 37
7.4 Mafanikio na Hitimisho ........ 38
8.0 UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA AFYA NGARA ........ 39
8.1 Utangulizi ........ 39
8.2 Hali ya Mradi Wakati wa Ufuatilaji ........ 39
8.3 Matokeo ya Ufuatiliaji ........ 41
8.4 Mapendekezo ........ 41
8.5 Mafanikio na Hitimisho ........ 42
9.0 THAMANI YA FEDHA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA INAYOSIMAMIWA NA TARURA WILAYANI LINDI ........ 43
9.1 Utangulizi ........ 43
9.2 Matokeo ya Ufuatiliaji ........ 44
9.3 Mapendekezo ........ 44
9.4 Mafanikio na Hitimisho ........ 45
10.0 MATUMIZI YA 'FORCE ACCOUNT' KATIKA UJENZI WA KITUO CHA AFYA MNAZI MMOJA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ........ 46

10.1 Utangulizi ........................................................................................................ 46

10.2 Matokeo ya Ufuatiliaji ........................................................................................ 47

10.3 Mapendekezo........................................................................................................ 49

10.4 Mafaniko na Hitimisho ........................................................................................ 50

11.0 MIANYA YA RUSHWA KATIKA UNUNUZI NA USAFIRISHAJI WA ZAO LA UFUTA KATIKA WILAYA YA NACHINGWEA ................................................ 52

11.1 Utangulizi ........................................................................................................ 52

11.2 Matokeo ya Uchambuzi ........................................................................................ 53

11.3 Mapendekezo........................................................................................................ 53

11.4 Mafanikio na Hitimisho ........................................................................................ 55

## OROGHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AfDB | - | African Development Bank |
| AMCOS | - | Agricultural Marketing Cooperative Societies |
| BOQ | - | Bills of Quantities |
| CEO | - | Chief Executive Officer |
| DED | - | District Executive Director |
| DFID | - | UK Department for Internationla Development |
| DP | - | Development Pertiners |
| EFD | - | Electronic Fiscal Devices |
| GN | - | Government Notice |
| KU | - | Kamati ya Usimamizi |
| LGRCIS | - | Local Government Revenue Collection Information System |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza na Umaskini Tanzania |
| MTEF | - | Medium Term Expenditure |
| OPD | - | Out Pertiant Department |
| POS | - | Point of Sale |
| RAS | - | Reginal Administrative Secretary |
| TAKUKURU | - | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANESCO | - | Tanzania Electrical Supply Company |
| TANROADS | - | Tanzania National Roads Agency |
| TARURA | - | Tanzania Rural Roads Authority |

| | | |
|---|---|---|
| TASAF | - | Tanzania Social Action Fund |
| TFS | - | Tanzania Forest Service Agency |
| TRA | - | Tanzania Revenue Authority |
| VEO | - | Village Executive Officer |
| VFM | - | Value for Money |
| WB | - | World Bank |
| WEO | - | Ward Executive Officer |

## 1.0 MFUMO WA UKUSANYAJI MAPATO KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI

### 1.1 Utangulizi

Ukusanyaji wa mapato ni moja ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano. Lengo la Serikali ni kujenga uwezo wa ndani wa kujitegemea na kupunguza kwa kadri inavyowezekana utegemezi kutoka kwa Wadau wa Maendeleo (DPs) na kuhakikisha kuwa mipango ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini inatekelezwa bila kukwama. Aidha, azma ya Serikali ya kuifanya Tanzania nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, haiwezi kufikiwa endapo Serikali haitokuwa na uwezo wa kifedha wa kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo. Takwimu zilizopo zinaonesha tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani mwaka 2015, kumekuwepo na ongezeko la makusanyo kwa mwezi kutoka shilingi za Kitanzania bilioni 800 (Bilioni mia nane) hadi kufikia shilingi za Kitanzania Trilioni 1.3 (Trilioni moja na bilioni tatu) kwa mwezi kutokana na mwitikio chanya wa wananchi wa kulipa kodi, usimamizi katika ukusanyaji mapato na kuzibwa kwa mianya ya upotevu. Mifumo ambayo imeanzishwa na Serikali ni pamoja na 'Local Government Revenue Collection Information System' (LGRCIS) na 'Point of Sale' (POS). Lengo la mifumo hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

Hata hivyo, bado yamekuwepo malalamiko kutoka kwa wadau kama vile wasomi, watunga sera, watendaji na wananchi wa kawaida kuwa  mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (Point of Sale) zimeshindwa kuongeza mapato ya Serikali kama ilivyotarajiwa na kwamba sababu za Serikali kuendelea kupoteza mapato,  hata baada ya kuanza kutumika rasmi kwa mashine za 'POS' mwaka 2016, bado haziko wazi. Kwa sababu hiyo, TAKUKURU iliona kuna haja ya kufanya uchambuzi wa mfumo wa 'POS' ili kubaini endapo kuna mianya ya rushwa inayosababisha upotevu wa mapato ya Serikali na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuziba mianya hiyo. Uchambuzi huu ulifanyika katika mikoa 20 ya Tanzania bara kwa kuchagua halmashauri 32 kutoka katika mikoa hiyo. Mikoa hiyo ni Tanga, Tabora, Geita, Arusha, Mbeya,

Dodoma, Shinyanga, Lindi, Morogoro, Mwanza, Kagera, Ruvuma, Dar es Salaam, Mara, Pwani, Singida, Manyara, Njombe, Rukwa na Kilimanjaro.

### 1.2 Matokeo ya Uchambuzi

Uchambuzi huo ulibaini mambo yafuatayo:

i. Uwepo wa idadi ndogo ya mashine za kukusanya mapato (POS) kinyume na mahitaji halisi katika halmashauri nyingi nchini. Mfano katika halmashauri ya Bahi ilikuwa na mashine za 43 tu wakati mahitaji halisi yalikuwa 150, Biharamulo kulikuwa na mashine za 'POS' 56 wakati mahitaji halisi ni 'POS' 92, Handeni kulikuwa na mashine za 'POS' 16 wakati mahitaji halisi ni 'POS' 25. Matokeo yalionesha kwamba mashine zilizokuwepo hazitoshelezi mahitaji halisi na watendaji wasio waadilifu hutumia mwanya huo kujinufaisha.

ii. Kuna usimamizi dhaifu wakati wa kuzipokea, kuzihifadhi na kuzigawa mashine za 'POS' kwa watumiaji. Taratibu zinataka mashine hizi kuwa chini ya usimamizi wa idara ya fedha. Hata hivyo, uchambuzi ulibaini kwamba baada ya mashine kununuliwa na kuziingiza katika vitabu vya halmashauri, mashine hizo hukabidhiwa watumishi wa Idara ya TEHAMA. Mashine hizo kukabidhiwa kwa idara ya Tehama badala ya Idara ya Fedha, inapunguza uwajibikaji wa Mweka Hazina ambaye ndiye mwenye dhamana ya kusimamia fedha za Halmashauri. Ni vigumu kwa Mweka Hazina kupata taarifa kamili ya kile kinachoendelea kwenye Mfumo. Pia ulibaini kuwa mashine hizo hubakia mikononi mwa wataalamu wa TEHAMA badala ya kuhifadhiwa kwenye chumba Maalum (Strong Room).

iii. Kutokana na uhaba wa watumishi katika halmashauri nyingi hapa nchini, mashine za 'POS' kuna nyakati askari wa jeshi la akiba yaani mgambo au vibarua hukabidhiwa mashine za 'POS' ambao kimsingi si watumishi wa halmashauri na hawabanwi na mkataba wowote ule kama vile ilivyo kwa Watendaji wa Kata (WEOs), Watendaji wa Vijiji (VEOs), Maafisa mifugo (Veternary Officers), Maafisa Afya (Health Officers) na wengine walipewa jukumu la kukusanya mapato katika maeneo yao. Kwa kutambua kuwa hawabanwi na mkataba wowote,

askari mgambo/vibarua kwao ni rahisi kuzitumia mashine hizo vibaya (abuse instead of using).

iv. Hakuna utaratibu au maelekezo maalum yanayoeleza lini fedha zilizokusanywa zinapaswa kuwasilishwa benki. Hali hii husababisha watumishi wanaokusanya mapato kukaa na fedha kwa muda mrefu bila kuziwasilisha benki. Taarifa ya tathmini ya ufuatiliaji wa makusanyo ya mapato inaonesha kuwa Mhasibu wa Mapato wa halmashauri ya Wilaya ya Karagwe alichukuwa shilingi 23,261,400/= [shilingi million ishirini na tatu laki mbili na sitini na moja na mia nne] kwa nyakati tofauti kutoka kwa wakusanyaji na kushindwa kuziwasilisha fedha hizo kwa wakati kwenye akaunti. Vilevile, taarifa hiyo inaonesha kuwa askari mgambo mmoja kwenye kizuizi alikusanya Tsh. 200,000 [Shilingi laki mbili] na kushindwa kuziwasilisha kunakotakiwa na hakuna hatua zozote alizochukuliwa. Pia Mhasibu wa Mapato wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo naye alichukua Tsh. 4,220,000/= [Shilingi milioni nne na laki mbili na ishirini] kutoka kwa wakusanyaji tofauti na kushindwa kuziwasilisha kwenye akaunti ya Halmashauri

v. Baadhi ya Wakurugenzi Watendaji wa halmashauri hawana utaratibu mzuri wa kupata taarifa za makusanyo ya mapato. Matokeo yake ni kwamba wadaiwa katika mfumo wa kukusanya mapato wamekuwa hawajadiliwi kwenye vikao vya Halmashauri, watendaji uamua kubadilisha namba za utambulisho wa mashine za ‘POS’ bila kupata kibali cha kufanya hivyo, kupotea kwa kumbukumbu za miamala ya makusanyo pale ambapo mashine za ‘POS’ zinakuwa hazifanyi kazi, baadhi ya wakusanyaji kupunguza kiasi cha fedha kinachopaswa kukusanywa na kuwasilisha benki fedha zikiwa pungufu.

vi. Baadhi ya mashine za ‘POS’ hazifanyi kazi kama inavyotakiwa kutokana na matatizo ya kiufundi [technical defects]. Pia ulibaini kuwa katika utayarishaji wa risiti, kuna baadhi ya risiti hukosa kumbukumbu muhimu kama vile jina la mlipaji au huduma iliyolipiwa ushuru, hazioneshi tarehe, namba na ‘batch’kwenye risiti.

vii. Mashine nyingi za ‘POS’ hazina muunganiko mzuri na mifumo mingine mikubwa kama vile ‘LGRCIS’, GOT-HOMIS na Benki. Kukosekana kwa muunganiko huo kunafanya zoezi la usuluhishi [reconciliation] kuwa gumu na kutoa mwanya kwa baadhi ya wakusanyaji wa mapato kuchepusha sehemu ya mapato.

viii. Hakuna utaratibu mzuri wa makabidhiano ya mashine za ‘POS’. Hakuna taarifa za kubadilishana ‘PASSWORD’ pale mtumishi anapokuwa nje ya kituo cha kazi na hivyo kuwa rahisi kwa mtu mwingine yoyote kutumia mashine ya ‘POS’ kwa urahisi bila kuwa na kiwazo chocho te.

ix. Marekebisho ya miamala (bank reconcilliation) hufanyika katika mfumo bila kupata kibali au idhini ya Afisa Maduhuli [CEO] au bila kuwa na uthibitisho wa nyaraka (Journal Vouchers) unaonesha sababu za kufanya hivyo.

x. Hati za Madai [Bill] nyingi anazopewa mkusanyaji hazioneshi kipindi maalum ambacho fedha inayopelekwa benki imekusanywa.

xi. Baadhi ya wakusanyaji kwa sababu wanazozijua wao huzima mashine za ‘POS’ na kufanya miamala au nyakati nyingine huamua kuweka kadi zao za simu (Sim Card) na kukusanya fedha kinyume na taratibu za Serikali.

xii. Baadhi ya wafanyabiashara wamegundua kuwa njia rahisi ya kukwepa kodi ni kusafirisha mizigo nyakati za usiku kwa vile watumishi wengi wanakuwa hawapo kwenye vizuizi wakati huo.

xiii. Watendaji wasio waadilifu hudanganya kuwa walikosea kuingiza tarakimu za namba kwenye ‘POS’ na hivyo kulalamikia hati za madai wanazopewa na kusema kuwa si sahihi. Mfano akiingiza 50,000/= husema alikosea alikusudia kuingiza 5,000/- ili wachepushe sehemu ya mapato kwa manufaa yao binafsi.

xiv. Watumiaji wengi wa mashine za ‘POS’ hawajui kuzitumia mashine hizo. Watumishi wachache tu ndio walipata mafunzo rasmi ya namna ya kutumia mashine hizo. Pia watendaji walio wengi hawatumii ‘POS’ wao wenyewe na badala yake huwakabidhi vijana ambao hawana uelewa wa kuzitumia kwa ahadi ya kupewa’ kitu kidogo’ baadaye.

xv. Asilimia kubwa ya maeneo zilipo ‘POS’ yanakabiliwa na upungufu wa mtandao wa uhakika. Kitaalamu maeneo mengi hali ya mtandao ni kiwango cha chini yaani “E” ili hali “LGRCIS app” kusukuma miamala kwenye mfumo mkubwa kwa uhakika inahitaji mtandao kiwango cha “3G”, “4G”, “H”na “H+”. Hali hii ya ukosefu wa mtandao maeneo mbali mbali inaathiri kwa kiwango kikubwa zoezi la uwasilishaji wa makusanyo, inaweza tumia muda kuanzia masaa matano hadi siku tatu ‘POS’ ya husika kusoma kwenye mfumo mkubwa. Hii inatoa mwanya kwa watendaji wasio waadilifu kusingizia mtandao hata kama sio kweli na kujinufaisha wao. Aidha, hali hii husababisha wakusanya mapato kukusanya mapato bila ya kutoa stakabadhi na kuahidi watatoa stakabadhi baadae, lakini hakuna stakabadhi inayotolewa baada ya mlipaji kuondoka, na hii husababisha kukosekana kwa kumbukumbu ya makusanyo na kutoa mwanya kwa muhusika wa makusanyo kuchepusha mapato.

### 1.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya uchambuzi huo, Taasisi ilipendekeza mambo yafuatayo ili kuziba mianya ya rushwa na kudhibiti upotevu wa mapato:-

i. Wakurugenzi watendaji waweke utaratibu wa kupewa taarifa za makusanyo kila wiki na taarifa hizo zioneshe kiasi halisi kinachodaiwa kila mkusanyaji.

ii. Taarifa za wakusanyaji wanaodaiwa ziwe zinajadiliwa kwenye vikao vya Menejimenti vya kila mwezi ili kudhibiti upotevu wa mapato

iii. Ili kuweka kumbukumbu vizuri, Halmashauri zote zianzishe ‘Rejista’ kwa ajili ya mashine za ‘POS’ na kuhifadhiwa kwenye chumba maalum (strong room).

iv. Wakusanyaji wa mapato wakabidhiwe mashine za ‘POS’ kwa barua ya Mkurugenzi yenye maelekezo mahsusi ya namna mashine hizo zinapaswa kutumiwa, uwasilishaji wa makusanyo benki na hatua zinazoweza kuchukuliwa endapo kutakuwa na ukiukwaji wa maelekezo.

v. Pale ambapo kuna ulazima wa kuwatumia askari wa akiba [Mgambo] au vibarua, makabidhiano ya mashine hizo [POS] yafanyike kisheria na kwa sababu hiyo mwanasheria wa halmashauri asaidie katika suala hili kuliko hali ilivyo sasa ambapo mgambo hukabidhiwa bila kuwepo kwa maandishi yoyote yanayombana.

vi. Kuwekwe muda maalumu wa kuwasilisha makusanyo yote benki na watendaji watakaochelewa kupeleka fedha benki bila sababu za msingi hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao

vii. Wakuu wa Idara za Fedha wawe wanafanya usuluhishi mapema iwezekanavyo na kutoa taarifa kwa Afisa Masuuli. Wadaiwa wote wapatiwe hati za madai kwa maandishi na fedha zipelekwe benki.

viii. Halmashauri zitenge bajeti kwa ajili ya kuwanunulia watendaji vifurushi vya mtandao ili kutatua changamoto za upatikanaji wa mtandao kwenye baadhi ya maeneo

ix. Uwekwe utaratibu mzuri wa kuhamisha mashine za ‘POS’ kutoka kwa Afisa mmoja kwenda kwa mwingine ili kudhibiti makabidhiano holela ya mashine hizo kama ilivyo sasa

x. Taarifa zote za mapato zinazopelekwa kwenye vikao vya halmashauri zichukuliwe kutoka kwenye mfumo rasmi wa ‘LGRCIS’.

xi. Ukusanyaji wa mapato kwa kutumia risiti za mikono usitishwe na endapo kuna sababu za msingi ya kufanya hivyo, basi Afisa Masuhuli ajulishwe na akiridhika ndiye atakayekuwa na mamlaka ya kutoa kibali.

xii. Halmashauri ziendelee kuwaelimisha watumiaji wa ‘POS’ ili kuboresha utendaji wao.

xiii. Kuimarisha kwa ulinzi na usimamizi kwenye vizuizi hasa nyakati za usiku ili kudhibiti tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kukwepa kulipa ushuru

### 1.4 Mafanikio na Hitimisho

Mfumo wa ‘POS’ ukitumiwa vizuri utasaidia kuziba mianya yote ya rushwa na mapato ya Serikali yataongezeka na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Ni dhahiri tukijenga uwezo wetu wa ndani kifedha tutapunguza utegemezi wa kutoka nje. Serikali imedhamiria kufikia uchumi wa kati, suala la ukusanyaji wa mapato na kudhibiti vitendo vyote vya rushwa, wizi na ufisadi linapaswa kupewa uzito unaostahili. Baada ya ufuatiliaji huu, Katibu Mkuu –Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) alimwandikia Mkurugenzi Mkuu akiahidi kuchukua hatua za kuzuia aina zote za rushwa katika ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki (POS). Aidha, uongozi wa TAMISEMI wameonesha utayari wa kushirikiana na Taasisi kwa kuwatumia wataalamu wake kuwafundisha wachunguzi kutoka TAKUKURU ili kuwajengea uwezo.

## 2.0 MIANYA YA RUSHWA KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA USAFIRI WA UMMA JIJINI DAR ES SALAAM

### 2.1 Utangulizi

Utoaji wa huduma bora za jamii ni jukumu la msingi la Serikali zote duniani. Kodi ndio chanzo muhimu cha mapato kinachoziwezesha Serikali kutoa huduma bora za kijamii. Hivyo, Serikali ya Tanzania imechukua hatua za makusudi za kuanzisha miradi mikubwa ya kutoa huduma za usafiri na maegesho katika jiji la Dar-es-Salaam. Miradi hiyo ni mabasi yaendayo kasi, Treni inayotoa huduma jijini, kituo cha mabasi Ubungo na maeneo ya maegesho ya magari. Lengo kuu la kuanzisha miradi hii ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za uhakika wakati wa kwenda na kurudi toka kwenye shughuli zao za uzalishaji za kila siku. Ili kuhakikisha miradi hiyo inajiendesha yenyewe na inakuwa endelevu, wananchi hutakiwa kuchangia huduma hizo. Lengo la utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kumudu gharama za uendeshaji kama vile mishahara ya watumishi pamoja na kugharamia matengenezo ya miundombinu yake. Hata hivyo, mapato yanayotokana na miradi hiyo yasiposimamiwa vizuri kwa sababu ya rushwa, si tu kwamba miradi hiyo itashindwa kujiendesha yenyewe, lakini pia azma ya Serikali ya kuwaletea maendeleo wananchi wake haitafanikiwa.

Usafiri wa umma ni kichocheo muhimu cha kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Huduma za usafiri katika miji mikubwa unawawezesha watu kufika kwenye maeneo yao ya kazi kwa wakati, kufanya biashara zao kwa ufanisi, kuyafikia masoko bila kikwazo, husaidia matumizi bora ya rasilimali muda na kurahisisha mawasiliano.  Ni dhahiri kuwa endapo muda mwingi utapotea njiani wakati wa kusafiri kutoka eneo mmoja kwenda lingine, shughuli nyingi za uzalishaji zitakwama na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika nchi zinazoendelea kama Tanzania. Kwa kuwa taarifa zilizopo ni finyu na hazielezi kwa kina tatizo la Serikali kukusanya mapato kinyume na matarajio yake; na kwa kuwa yapo malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wa sekta ya usafiri, kuwa usimamizi wa miradi hiyo hauridhishi na matokeo

yake kusababisha Serikali kukusanya mapato chini ya kiwango kinyume na matarajio, TAKUKURU iliona kuna umuhimu wa kufanya utafiti katika maeneo ya kimkakati jijini Dar es salaam kubaini mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato na kisha kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuiziba. Sababu ya kuchagua eneo la Dar es Salaam ni kwamba miradi hii inatekelezwa katika jiji la Dar es Salaam na taarifa muhimu ambazo zingeweza kusaidia kujibu maswali ya utafiti zilikuwa zinapatikana kwa urahisi jijini Dar-es-Salaam.

## 2.2 Matokeo ya Utafiti

### 2.2.1 Kukinzana kwa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ukusanyaji wa Mapato

Kuhusu usimamizi wa sheria, kanuni, taratibu katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato**,** utafiti ulibaini uwepo wa migongano ya kisheria (conflicting laws) katika ukusanyaji wa mapato ya ushuru wa maegesho ya magari jijini ambapo sheria mbalimbali zinatoa mamlaka kwa wakusanyaji tofauti katika maeneo yale yale. Sheria zifuatazo zinatoa mamlaka ya kukusanya mapato: (a) kifungu cha 29 cha Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007 inatoa mamlaka ya makusanyo ya fedha za maegesho/faini kwa Wakala wa Barabara TARURA na TANROADS; (b) vifungu namba 29 na 31 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 navyo vinatoa mamlaka kwa Halmashauri za Serikali za Mitaa/Manispaa/Majiji kukusanya mapato yakiwemo fedha za maegesho na stendi kwa kutumia mawakala; (c) waraka namba 16 wa 2016 wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Wakuu wa Mikoa (Tanzania Bara) kuhusu makusanyo ya mapato, matumizi ya mifumo ya kielektroniki (POS) katika ukusanyaji wa mapato na maeneo ambayo Serikali itatumia mawakala ambapo aya ya 6(ii) inazitaka Halmashauri kukusanya mapato yatokanayo na ada za maegesho ya magari na ushuru wa stendi. (d) Barua ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye kumb. Namba DA.347/371/01/13 ya 2018 kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa (Tanzania Bara) kuhusu makusanyo ya mapato yatokanayo na matumizi ya hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TARURA. Aidha, barua hiyo ilieleza kuwa, kwa mujibu wa kifungu namba 3 cha Sheria ya Barabara Namba 13 ya 2007, TARURA ni

Mamlaka ya Barabara na kwamba kifungu namba 29 kinaipa mamlaka TARURA kukusanya mapato kutokakana na ushuru wa maegesho ya magari ndani ya hifadhi ya barabara.

Vilevile ilibainika kuwa sheria na miongozo hiyo inaruhusu ukusanyaji wa mapato/ ada za maegesho ya magari mijini kufanywa na zaidi ya Mamlaka moja katika maeneo hayo hayo na hivyo kusababisha migongano ya kiutendaji kati ya taasisi moja na nyingine. Mathalan, kwa mujibu wa Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam ya GN 354 ya 2009, jiji linayo mamlaka ya kisheria ya kukusanya mapato katika maeneo yote ya Jiji. Wakati huo huo wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) inayo mamlaka kisheria ya kukusanya ushuru/ada ya maegesho ya magari katika maeneo ya hifadhi ya barabara za vijijini/mitaa ambazo hazipo katika hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TANROADS (Trunk roads). Pia kwa upande wa TANROADS, ilibainika kwamba taasisi hiyo imekuwa ikikusanya mapato yatokanayo na: (i) faini kutokana na ukiukwaji wa maegesho ya magari katika maeneo ya hifadhi ya barabara yasiyo ruhusiwa kisheria (wrong parking) na; (ii) upangishaji wa maeneo ya hifadhi ya barabara kwa watu binafsi kwa hifadhi za barabara inazosimamia na kuanzisha maeneo ya maegesho ya magari. Huu ni mgongano wa kiutendaji.

Ilibainika pia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inaendelea kutumia Sheria ndogo ya 2009 (Tangazo la Serikali Namba 354 la 23/10/2019) ya kukusanya mapato kwa Kituo Kikuu cha Stendi ya Mabasi ya Ubungo pamoja na maegesho ya magari lakini Sheria hiyo ilifutwa kwa kifungu namba 21 cha Sheria ndogo ya Tangazo la Serikali Namba 41 la 24/2/2017. Matumizi ya Sheria iliyofutwa inachangia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuendelea kupoteza mapato kutokana na baadhi ya ada kurekebishwa na kuongezewa kiwango tofauti na Sheria ndogo iliyofutwa ingawa bado inaendelea kutumika. Kwa mfano, Sheria ndogo ya 2009 iliyofutwa inaelekeza kuwa gharama za kulaza magari madogo ya mizigo katika kituo Kikuu cha Stendi ya mabasi Ubungo ni Tsh. 2000/- kwa siku wakati Sheria ndogo ya mwaka 2017 inaelekeza kuwa gharama za kulaza magari madogo ya mizigo (pick-ups) kwa siku ni Tsh.3000/-.

Utafiti ulibaini kuwa licha ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, vifungu namba 6(1) na 16(1) kuzipa Mamlaka Serikali za Mitaa ya kukusanya kodi kupitia Sheria ndogo wanazoziandaa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inatumia Sheria ndogo ya 2009 kukusanya mapato ya maegesho ya magari katika manispaa zote tano zinazounda Jiji la Dar es Salaam (Ubungo, Temeke, Ilala, Kinondoni na Kigamboni). Kiuhalisia, Manispaa hizi zinazounda Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam nazo zina mamlaka kisheria ya kupanga vyanzo vya makusanyo ya mapato katika maeneo yao (Rejea Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, vifungu namba 6(1) na 16 (1)).

Utafiti ulibaini kuwepo kwa usimamizi dhaifu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo unaochangiwa na migongano ya kisheria na uzembe wa baadhi ya watendaji kushindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mikataba baina ya halmashauri na mawakala. Aidha, utafiti ulibaini kuwa kuna watu binafsi ambao wameanzisha maegesho katika hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TANROADS na hawatumii mashine za kielektroniki na kwa sababu hiyo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa haikusanyi mapato kwa madai kwamba maeneo husika ni mali ya TANROADS.

### 2.2.2 Udhaifu katika Ukusanyaji wa Mapato Kituo cha Mabasi Ubungo

Kuhusu ufanisi wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato ya Serikali, utafiti ulibaini kuwa mifumo hiyo bado haijaweza kuongeza ukusanyaji wa mapato kama ilivyotarajiwa. Mfano, ilibainika kuwa katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo, kuwa mageti yote saba (7) na vyoo hakuna mashine hata moja ya ‘POS’. Maelekezo ya Serikali yanawataka wakusanya ushuru wote kutumia risiti za kielektroniki na si vinginevyo. Hata hivyo, ilibainika kuwa idara ya uhasibu kwa kushirikiana na baadhi ya wakusanya ushuru/ada katika maeneo ya getini, chooni na sehemu nyingine za huduma, si tu hawatumii mashine za kielektroniki lakini pia wamekuwa wakiuza tiketi za tarehe zilizopita ili kuiibia Serikali na mauzo ya risiti hizo hufanyika mapema alfajiri. Utafiti ulibaini kuwa watumishi katika kituo cha mabasi cha Ubungo

hutumia tiketi ambazo hazioneshi muda wala tarehe ambao mteja alipata huduma. Ilibainika kuwa watumishi wanaokusanya ushuru hupokea fedha pungufu kutoka kwa wateja, hawatoi risiti, huuza tiketi mara mbili na hubakiza risiti kwa lengo la kukusanyia ushuru ambao hautambuliwi na halmashauri ya jiji. Utafiti ulibaini kutotumika kwa mfumo wa kieletroniki wa kukusanya mapato katika mageti yote saba na hakuna usimamizi mzuri wa magari yanayolala ndani ya stendi kumesababisha upotevu wa mapato.

Utafiti ulitumia pia njia ya kushuhudia namna ukusanyaji wa mapato unavyofanyika siku za tarehe 5-6 Novemba 2018, na kubaini yafuatayo: (a) kuna usimamizi mbaya wa makusanyo getini na kutokuwepo kwa mfumo wa kielektroniki wa kuhesabu mabasi yaliyolala stendi ili kulipa ada/ushuru stahiki kabla ya kuondoka stendi na*;* (b) kwamba siku ambazo TAKUKURU ilisimamia ukusanyaji wa ushuru getini, mapato yaliongezeka katika kituo cha mabasi cha Ubungo kutoka Tsh.6,933,100 hadi Tsh.7,321,800/- kwa siku, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 388,700. Hata hivyo, baada ya TAKUKURU kuondoka ukusanyaji wa mapato ulishuka tena hadi kufikia Tsh.6,768,900 (ikiwa ni tofauti ya Tsh.552,900/- kwa siku), na (c) hakuna mfumo mzuri wa kudhibiti watu wanaoingia na kutoka ndani ya kituo hicho ambako si tu huikosesha Serikali mapato bali pia inaweza kuhatarisha usalama wa abiria na mali zao.

Utafiti ulibaini kuwa Uongozi wa jiji la Dar-es-salaam umekuwa ukikusanya mapato chini ya matarajio katika kituo cha mabasi cha Ubungo. Mfano, matarajio ya makusanyo ya Jiji la Dar es Salaam kwa mwaka 2018/2019 katika kituo cha mabasi cha Ubungo yalikuwa ni Tsh. 2,399,855,805 (wastani wa Tsh.199, 987,983/-kwa mwezi). Hata hivyo, makusanyo ya juu yaliyokuwa ni Tsh. 71,621,360 na ya chini ni Tsh. 24,514,650. Matokeo yalionesha kwamba halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam linapoteza mapato katika kituo cha Ubungo kutokana na kutozingatiwa kwa matumizi sahihi ya kukusanyia fedha kwa njia ya kielektroniki (POS).

### 2.2.3 Ukiukwaji wa Mikataba ya Maegesho ya Magari

Kuhusu mapato yanayotokana na maegesho ya magari, ilibainika kuwa katika kipindi cha 2017/2018, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliingia mikataba na mawakala ‘M/S Excel

Accountancy Services Limited' mnamo tarehe 1 /02/2018 na 'M/S Chui Systems Limited' tarehe 26/01/2018. Matokeo yalionesha kuwa kwa kipindi cha kuanzia Februari 2018 na Novemba 2018 mawakala hao walikiuka makubaliano ya mkataba wa uwasilishaji wa mapato kwa mwezi na hakuna hatua iliyochukuliwa dhidi yao. Mathalani, 'M/S Excel Accountancy' kwa mujibu wa mkataba alitakiwa kuwasilisha kiasi cha fedha Tsh.716,050,000 kwa mwezi na M/S Chui Tsh.219,445,270.21 kwa mwezi. Hata hivyo, takwimu zinaonesha wakala 'M/S Excel Accountacy' ametekeleza makubaliano kama yalivyoainishwa kwenye mkataba kwa kipindi cha miezi miwili tu (yaani mwezi Mei na Julai, 2018); wakati 'M/S Chui Systems Limited' yeye hakuwahi kutekeleza masharti ya mkataba. Ilibainika pia kuwa wakusanya ada/ushuru katika baadhi ya maeneo ya maegesho ya magari walikuwa hawatumii risiti za kielektroniki wanazopewa na wasimamizi wao kinyume na utaratibu.

### 2.2.4 Mianya ya Rushwa katika Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Uwepo wa utitiri wa sheria na miongozo kinzani zinazosimamia ukusanyaji wa mapato katika eneo moja. Sheria na miongozo hiyo ni pamoja na Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Tangazo la Serikali 41 la mwaka 2017 na Tangazo la Serikali namba 354 la 2009; Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007 inayosimamiwa na TANROADS na TARURA; Vifungu namba 29 na 31 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; Barua ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye Kumb. Namba DA. 347/371/ 01/13 27 ya tarehe 27 Juni, 2018 na; Waraka namba 16 wa 2016 (CAB:110/156/01/26 wa 11 Julai 2016) wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Wakuu wa Mikoa (Tanzania Bara) na; barua ya Mtendaji Mkuu wa TARURA kwenda kwa Waratibu wa TARURA Mikoa Tanzania Bara, barua yenye Kumb. Namba CAC.310/338/01/02 ya 29/6/2018 na; Barua ya Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dar es Salaam kwenda Mkurugenzi wa Jiji kuhusu Mapato yatokanayo na hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TARURA (TRR/DRC/M.13/7/2 ya 4/7/18). Utafiti umebaini kuwa Sheria na miongozo husika zinaruhusu ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ya magari kama vyanzo vya mapato katika Halmashauri za Serikali za Mitaa ikiwemo Jiji la Dar es Salaa na kusababisha

migongano kati ya taasisi moja na nyingine (Rejea vifungu Na. 29 na 31 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, Sheria ya Barabara Namba 13 ya 2007)

Ukiukwaji wa makusudi wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia ukusanyaji wa mapato unaofanywa na baadhi ya watendaji wasio waadilifu kwa lengo la kujinufaisha binafsi pasipo kuzingatia maslahi ya umma. Mfano, kitendo cha viongozi wa kituo cha mabasi cha Ubungo kugawa tiketi kwa wakusanya ushuru bila kuwapa mashine za 'POS', kitendo cha baadhi ya watumishi/wakusanya ushuru kuuza tiketi ambazo zimeisha matumizi yake, kitendo cha kutochukuliwa hatua stahiki kwa mawakala wanaoshindwa kutekeleza makubaliano ya uwasilishaji wa kiwango cha makusanyo ya fedha, kitendo cha watu binafsi walioanzisha maegesho ya magari baada ya kupangishwa na 'TANROADS' na kukata ushuru/ada bila kutumia mashine za 'POS' kwa pamoja vinathibitisha ukiukwaji wa makusudi wa sheria, kanuni na taratibu wenye lengo la kupoteza mapato ya Serikali.

Matumizi ya sheria na kanuni zilizopitwa na wakati. Mfano, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kukusanya ushuru ndani ya stendi ya Ubungo kwa kutumia Sheria Ndogo namba 354 ya mwaka 2009 (Toleo la 23/10/2009) badala ya kutumia Sheria Ndogo iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali (GN) Na. 41 la tarehe 24/02/2017 iliyofuta matumizi ya Sheria Ndogo ya mwaka 2009.

Kushindwa kusimamia vizuri mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Utafiti ulibaini kuna ukiukwaji wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato vikiwemo vitendo vya wizi na udanganyifu. Katika Kituo cha Ubungo ilibainika kwamba katika mageti yote 7 yaliyopo Stendi ya Ubungo hakukuwa na mashine yeyote ya kukusanyia mapato (POS) na pia mfumo wa kuhesabu magari yanayoingia, kulala na kutoka kituoni siyo wa kielektroniki na hivyo kuweka mazingira ya wizi na udanganyifu katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, Serikali imetoa mwongozo wa namna ya kuingia mikataba baina ya halmashauri na mawakala pamoja na msisitizo wa matumizi ya mashine za kielektroniki (POS) katika kukusanya mapato.

Tabia ya kuwasilisha mapato kiujumla bila kutoa mchanganuo unaoeleweka. Utafiti ulibaini kuwa kuna vyanzo vingi vya ukusanyaji wa mapato katika stendi ya mabasi Ubungo lakini uwasilishaji wa taarifa za makusanyo ya mapato ya kila siku hauoneshi mchanganuo wa kila chanzo na kiasi kilichokusanywa na hivyo kutoa mwanya kwa baadhi ya watendaji kujihusisha na vitendo vya wizi na udanganyifu.

Uholela na mpangilio mbaya wa biashara ndani ya stendi ya kituo cha mabasi cha ubungo. Utafiti umebaini hakuna utaratibu mzuri kuomba kufanya biashara ndani ya kituo cha mabasi, na hivyo kufanya kazi ya utambuzi wa wafanyabiashara kuwa ngumu.

Uuzaji wa risiti zilizopitwa na wakati saa kumi na moja alfajiri wakati tayari risiti hizo hazitakiwi kutumika tena. Matumizi ya risiti zilizokwisha muda wake unaingiza hasara Serikalini kwa kuwa risiti hizo huwa tayari zinahesabika kuwa zimerudishwa kwa mamlaka husika kwa lengo la kuweka mlinganisho (reconciliation) katika vitabu vya mahesabu ya mwajiri.

Kumekuwepo na vitisho toka kwa baadhi ya watumishi wa vyombo vya dola (extortion) dhidi ya viongozi wanaosimamia kituo cha mabasi cha Ubungo kwa kuwataka watoe ‘chochote’ vinginevyo watawachukulia hatua au kuwashughulikia. Vilevile, utafiti umebaini kuwa baadhi ya watumishi wa Jeshi la Polisi wamekuwa wakiomba kupewa huduma za chakula kwa gharama za kituo cha mabasi cha Ubungo.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, yafuatayo yalipendekezwa ili kuziba mianya ya rushwa iliyobainika:

i. Kufanya uchambuzi wa kina wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo zinazokinzana kwa lengo la kuainisha vifungu vinavyoingiliana/kugongana na kuzipatanisha (harmonize) kwa minajili ya kuondoa migongano ya kisheria kati ya taasisi moja ya umma na nyingine (Lack of coherence). Mipaka ya kiutendaji kati ya taasisi moja na nyingine iwekwe wazi kwa minajili ya kuondoa misuguano ya ki-taasisi isiyo kuwa ya lazima (institutional clashes).

ii. Kuimarisha usimamizi wa watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki hususan 'POS' na kuwachukulia hatua watumishi wasio waadilifu wanaohujumu mifumo ya kukusanya mapato kwa makusudi ili kujinufaisha.
iii. Kuanzisha uchunguzi wa ukukwaji wa matumizi ya mashine za kielektroniki (POS) katika kukusanya mapato katika vyanzo vya maegesho ya magari na kituo cha mabasi Ubungo Maafisa uchunguzi wa TAKUKURU wapewe 'Mafunzo Maalum' ya namna mashine za'POS' zinavyofanya kazi ili kuweza kubaini na kudhibiti hujuma.
iv. Elimu ya Mapambano dhidi ya rushwa iendelee kutolewa na wale wanaokakiuka sheria, kanuni na taratibu, na kujihusisha na vitendo vya rushwa hatua kali zichukuliwe mara moja dhidi yao bila woga wala upendeleo
v. Uongozi wa Halmashauri ya jiji l;a Dar es-salaam uimarishe usimamizi kwa kuhakikisha kila wakala anawasilisha makusanyo yote kwa wakati kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo; na kuchukua hatua kali kwa watakaokiuka ikiwemo kuwafikisha mahakamani kwa kosa la wizi. Ukusanyaji wa mapato uzingatie taratibu na miongozo ya Serikali kuhusu 'POS'.
vi. Kila mtumishi au wakala anapaswa kuwasilisha kiasi halisi kilichokusanywa kutoka katika kila chanzo bila kificho kwa ajili ya kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu utunzaji wa mahesabu na uwajibikaji
vii. Uongozi wa stendi ya kituo cha mabasi cha Ubungo uhakikishe unawatambua wafanyabiashara wote wanaofanya shughuli zao ndani ya kituo cha mabasi cha ubungo na kuimarisha usimamizi. Hii itarahisisha zoezi la ukusanyaji wa ushuru unaotokana na biashara hizo kuliko ilivyo sasa.
viii. Uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam utekeleze Sheria Ndogo ya 2017 badala ya 2009 iliyofutwa.

### 2.3 Mafanikio na Hitimisho

Nadharia za kiuchumi zinaonesha kuwa hakuna mbadala wa kodi na kwamba wananchi wanapaswa kulipa kodi kwa ustawi na maendeleo ya nchi zao. Kwa sababu hiyo basi, vitendo

vya rushwa, ubadhirifu, wizi katika mifumo ya ukusanyaji wa kodi ni lazima vidhibitiwe. Mifumo ya utoaji huduma inapaswa kufanyiwa tathmini za mara kwa mara ili kubainisha maeneo yenye udhaifu na kupendekeza hatua za kuiimarisha. Watendaji waliopewa dhamani ya kukusanya kodi wanapaswa kufanya kazi zao kwa uadilifu ili kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato. Mapendekezo yote hapo juu yaliwasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika ili kuchukua hatua zinazofaa kuziba mianya ya rushwa. Taasisi iliyopelekewa mapendekezo ya TAKUKURU ni TAMISEMI ambayo imeleta mrejesho kuwa tayari wameanza kuchukua hatua za kurekebisha dosari zote zilizobainishwa.

# 3.0 RUSHWA KATIKA HUDUMA ZITOLEWAZO NA VYAMA VYA MSINGI VYA KILIMO NA MASOKO (AMCOS) VYA ZAO LA KOROSHO NCHINI

## 3.1 Utangulizi

Korosho ni zao muhimu katika uchumi wa Tanzania likiwa miongoni mwa mazao maarufu ya biashara ulimwenguni. Zao hili linachangia karibu asilimia tano (5%) ya pato la Taifa na huchangia zaidi ya asilimia 10 ya fedha za kigeni zitokanazo na mauzo nje ya nchi. Ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa zao la korosho, vyama vya msingi vya kilimo na masoko (Agricultural Marketing Cooperative Societies) vilianzishwa ili kukabiliana na vikwazo vya ukosefu wa taarifa za bei za korosho na kiungo kati ya wakulima na soko; upatikanaji wa mikopo; huduma za ugani na dosari zingine za kimasoko. Pamoja na juhudi za Serikali za kukwamua ustawi wa wakulima wa korosho kwa kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Kilimo na Masoko, vyama hivi vimeendelea kulalamikiwa kwa kushindwa kutimiza malengo yaliyowekwa. Vyama hivi vimekumbwa na matatizo kadhaa ikiwemo matumizi mabaya ya fedha za vyama; wizi wa pembejeo, fedha na korosho; udanganyifu katika usimamizi wa fedha na uzito wa korosho zinazopokelewa katika maghala; kushusha ubora wa korosho zilizopokelewa katika maghala kwa kuchanganya korosho hizo na mawe au mchanga au korosho zenye ubora hafifu kwa lengo la watumishi/viongozi wa AMCOS kujinufaisha wenyewe, vitendo vya rushwa katika mapokezi ya korosho maghalani, usafirishaji wa korosho, malipo ya wakulima, mkopo ya pembejeo na upimaji wa korosho.

Kufuatia malalamiko haya, TAKUKURU ilifanya uchambuzi wa mfumo wa utoaji wa huduma wa Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) ili kuimarisha mfumo wa AMCOS nchini. Lengo kuu la uchambuzi likiwa ni kushauri mamlaka zinazohusika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa na udhaifu mwingine uliosababisha AMCOS kushindwa kutimiza malengo yake. Madhumuni mahsusi ya uchambuzi huu yalikuwa ni:- Kubaini mianya ya rushwa katika mfumo wa utoaji wa huduma wa AMCOS; Kubaini na kuainisha vikwazo vya utoaji huduma;

Kutathmini utendaji wa AMCOS na Kutoa ushauri wa namna ya kuimarisha mfumo wa utoaji huduma wa AMCOS. Uchambuzi huu ulifanyika katika mikoa ya Pwani (Mkuranga na Rufiji); Lindi (Nachingwea, Kilwa, Liwale); Mtwara (Newala, Nanyumbu, Tandahimba, Masasi); na Ruvuma (Tunduru). Taarifa za msingi zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali.

### 3.2 Matokeo ya Uchambuzi

Uchambuzi huo ulibaini yafuatayo:

i. Vitendo vya rushwa katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho unaohusiha yafuatayo:
ii. Upendeleo katika mapokezi ya korosho katika maghala ya kuhifadhia korosho tayari kwa kupelekwa katika minada;
iii. Usafirishaji wa korosho kutoka maghala ya AMCOS kwenda katika maghala makuu ambako minada ya korosho hufanyika. Baadhi ya wakulima hulazimika kutoa hongo ili korosho zao zipewe kipaumbele cha kupelekwa katika maghala makuu ili korosho zao ziuzwe mwanzo katika minada;
iv. Upimaji wa korosho wenye upendeleo unaohusisha kuongezea uzito wa korosho kwa njia za kidanganyifu wakulima waliotoa hongo;
v. Udanganyifu katika malipo ya wakulima;
vi. Baadhi ya wakulima na viongozi wa AMCOS hujihusisha na vitendo vya rushwa katika mchakato wa malipo ili walipwe pesa nyingi zaidi kuliko kiasi cha pesa ya korosho walizouza katika AMCOS husika kwa (a) kuchanganya mawe au mchanga katika korosho zilizopokelewa katika maghala au wakati wa kusafirisha korosho kutoka maghala ya vyama vya msingi vya ushirika kwenda maghala makuu ambako minada ya korosho hufanyika au wakati wa kusafirisha korosho nje ya nchi kwa lengo la kuongeza uzito ili wahusika wajinufaishe; (b) kupunguza uzito wa korosho za wakulima kwa kuiba korosho husika na kwa kisingizio kuwa korosho husika zilikauka zikiwa ghalani na hivyo kupungua uzito wake; (c) Kupokea korosho zisizo na ubora na/au zilizokataliwa katika minada iliyofanyika katika misimu iliyopita; (d) taarifa ya fedha kutoandaliwa kwa wakati; (e) Uwazi, ushirikishwaji na uelewa mdogo wa wadau wa zao la korosho; (f) uwepo wa biashara

haramu ya zao la korosho; na (g) uwepo wa viongozi wasio na sifa wenye wajibu wa kusimamia na kuendesha vyama vya ushirika vya kilimo na masoko (AMCOS). Mambo haya yote ni kinyume na sheria, kanuni na taratibu za 'AMCOS'

### 3.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya uchambuzi huo, taasisi ilipendekeza mambo yafuatayo ili kuziba mianya ya rushwa katika vyama vya ushirika, kilimo na masoko nchini (AMCOS):

i. Kuchukua hatua kali dhidi ya viongozi wa AMCOS wanaojihusisha na udanganyifu/wizi wa korosho, na upokeaji wa korosho zisizo na ubora,

ii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa ubora wa korosho ikiwemo ukaguzi wa kushtukiza katika maghala ya AMCOS na maghala makuu ambako minada hufanyika,

iii. Kufanya ukaguzi wa hesabu za AMCOS zote ili kuongeza dhana ya kuwajibika,Kusisitiza matumizi ya mizani sahihi ya kupimia korosho ambayo imekaguliwa na kuidhinishwa na Wakala wa Vipimo

iv. Vyama Vikuu vya ushirika vya mikoa na wilaya kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho viimarishe udhibiti wa ndani wa AMCOS kwa kuzingatia (a) Kuweka wazi mnyororo (chain) wa uwajibikaji; (b) kuimarisha mawasiliano ya ndani ya AMCOS na mawasiliano baina ya AMCOS na Vyama vikuu vya ushirika, Bodi ya Korosho na wadau wengine; (c) kuwapatia viongozi maelezo ya kazi zao (job description); (d) kuwepo, kutambulika na kutumika kwa Mkataba wa Huduma kwa Mteja; (e) kutoa elimu ya huduma bora kwa mteja; (f) kufanya tathmini ya utendaji wa viongozi wa AMCOS; na (g) ufanya ukaguzi wa kushtukiza mara kwa mara katika sehemu za kazi

v. Kuondoa ucheleweshaji wa malipo ya wakulima kwa: (a) kuchukua hatua dhidi ya viongozi wa AMCOS wanaoiba fedha na wanaochelewesha malipo ya wakulima; na (b) kuhakikisha kuwa kazi za AMCOS zinafanywa kulingana na sheria, kanuni na taratibu za vyama vya ushirika.

vi. Kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kuhakikisha kuwa pesa zote zinazotolewa na wakulima kupitia ushuru/makato zinakusanywa na mfumo rasmi wa AMCOS,

vii. Kusimamia, kusisitiza na kujenga utamaduni wa kuandaa taarifa za mapato na matumizi na kisha kuzisoma na kuzijadili katika mikutano ya wanachama/wadau

viii. Kuendeleza maadili, nidhamu na uwajibikaji wa viongozi wa AMCOS kwa : (a) kuunda, kutambua na kufanya kazi kwa Kamati ya Maadili; (b) kuweka wazi majukumu ya viongozi wa AMCOS; kutoa zawadi kwa viongozi bora na kuwaadabisha wakosaji, na;

ix. Kuandaa na kutekelza programu za mafunzo ya miundombinu ya maadili kwa viongozi/watumishi wa AMCOS

### 3.4 Mafanikio na Hitimisho

Vyama vya ushirika, kilimo na masoko vina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Vikisimamiwa vizuri na kudhibiti vitendo vya rushwa, wizi na ubadhirifu vitachochea ukuaji uchumi na kupunguza umaskini. Serikali inapaswa kuweka mifumo ya udhibiti na kuhakikisha kuwa malengo ya kuanzishwa kwa vyama hivi yanafikiwa. Elimu ya rushwa inapaswa kutolewa kwa viongozi na wanachama na kuwachukulia hatua wale watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Ni matumaini ya Serikali kuwa uadilifu, uwazi na uwajibikaji, weledi na uongozi bora ni baadhi ya mambo ya msingi ambayo viongozi wanapaswa kuyasimamia ili kufikia malengo waliyojiwekea. Ni dhahiri kuwa rushwa ikidhibitiwa, mafanikio yatapatikana. Taasisi iliwasilisha kwa wadau wa korosho matokeo ya ufuatiliaji na uongozi wa AMCOS kwa kushirikiana na wanachama wake umeahidi kuchukua hatua za kuzuia vitendo vya rushwa kwa kuimarisha usimamizi, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara [na wakati mwingine kufanya ukaguzi wa kushtukiza], kuendelea kutoa elimu ya rushwa na kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa bila hofu wala upendeleo.

## 4.0 TATHMINI YA UFANISI WA MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI KATIKA KUONGEZA MAPATO YA SERIKALI (EFDs)

### 4.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania ilianza kutumia mfumo wa kukusanya kodi kwa kutumia Mashine za Kielektroniki (EFDs) mwaka 2010. Hatua hii ilitokana na kuwasilishwa Bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2010) uliopendekeza kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (The Income Tax Act, Cap.332 (Electronic Fiscal Devices) na Kanuni zake za mwaka 2012. Pamoja na mambo mengine, lengo la kuanzishwa kwa matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato lilikuwa ni kuongeza mapato ya Serikali kwa kuhamasisha tabia ya ulipaji kodi, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na vitendo vya rushwa vilivyokuwa vikifanywa na baadhi ya watumishi wa umma wasio waadilifu kwa maslahi binafsi.

Takwimu zinaonesha kuwa tangu kuanza kutumika kwa mashine hizo, mapato ya Serikali yaliongezeka kwa asilimia 59 katika kipindi cha kuanzia Julai 2010 hadi Juni 2013. Katika kipindi cha 2009/2010 na 2010/2011 wastani wa makusanyo kwa mwezi yalikuwa ni Bilioni 756 na Bilioni 890 mtawalia. Kwa mujibu wa Mamlaka ya Mapato, katika kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2015/2016 na Julai hadi Desemba 2016/2017, makusanyo ya kodi yaliongezeka kutoka Trilioni 6.44 hadi kufikia Trilioni 7.27 mtawalia, ikiwa ni ongezeko la asilimia 13. Hata hivyo, licha ya mafanikio haya yaliyopatikana katika kipindi cha takribani miaka kumi iliyopita, bado matumizi ya mashine hizo hayajaweza kukuza tabia ya ulipaji kodi na kuongeza mapato ya Serikali kama ilivyotarajiwa. Ni kwa sababu hiyo, TAKUKURU ilifanya utafiti mdogo kwa lengo la kutathmini ufanisi wa mashine hizo katika kukuza tabia ya ulipaji kodi na kuongeza mapato ya Serikali.

## 4.2 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yamegawanyika katika sehemu mbili: (1) ilihusu mitazamo (perceptions) ya wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa kodi kuhusu uzingatiaji wa matumizi ya mashine za EFD na (2) ilihusu taarifa kutoka kwenye uwanda (field report) kama inavyoonekana hapa chini:

### 4.2.1 Mitazamo ya Wafanyabiashara Kuhusu Matumizi ya Mashine za Kielekroniki

Kuhusiana na mtizamo utafiti ulibaini yafuatayo:

i. Utafiti ulibaini kuwa zaidi ya 80% ya wafanyabiashara hawaungi mkono na wana mtazamo hasi (negative perception) kuhusu matumizi ya mashine hizo kwa madai kwamba wakizitumia mashine hizo kama inavyotakiwa kisheria hawawezi kupata faida. Kwa upande mwingine, makundi matatu yaliyosalia yaani wananchi, mawakala na baadhi ya wafanyabiashara walionesha mtazamo chanya na wanaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kukusanya mapato yake kwa kutumia mashine hizo.

ii. Kuhusu uwezo wa kuzitumia mashine za kielektroniki, ilibainika kuwa 63% ya wana uwezo wa wafanyabiashara wana uwezo wa kuzitumia mashine hizo kinyume na dhana ilijengeka kuwa Serikali haikusanyi mapato ya kutosha kwa sababu watumiaji (wafanyabiashara) hawajui kuzitumia mashine za EFDs. Wahojiwa 70% walieleza kwamba wanafahamu kuzitumia mashine hizo isipokuwa Serikali haikueleza kwa kina sababu za kuanza kuutumia mfumo mpya wa mashine za kielektroniki na kuacha matumizi ya mfumo wa zamani wa risiti za mkono waliokuwa wameuzoea. Aidha, wahojiwa walieleza kuwa Serikali ilitumia utaratibu wa kuagiza na kuelekeza na sio kushirikisha (Top down style). Utafiti ulibaini kuwa kutoshirikishwa kwa kundi la wafanyabiashara kumechangia wengi wao kuwa na mtazamo hasi kuhusu matumizi ya mashine hizo.

iii. Kuhusu sababu za wafanyabiashara kutozingatia Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ilibainika kuwa, pamoja na mambo mengine, vitendo vya rushwa na tamaa ya kupata utajiri

wa haraka kwa baadhi ya watumishi wa umma vinachochea ukiukwaji wa makusudi wa sheria mbalimbali za kodi.

iv. Kuhusu ufanisi wa mashine za kielektroniki katika kuzuia vitendo vya rushwa, ilibainika kuwa 100% ya mawakala wanakubali kuwa EFDs zimesaidia kuzuia vitendo vya rushwa, 70% ya wafanyabiashara walihojiwa walikubali kuwa zimesaidia kudhibiti rushwa. Aidha, 70% ya wananchi waliohojiwa wanakubali kuwa zimesaidia kuwadhibiti watendaji waliokuwa wamezoea kujinufaisha kwa kuiibia Serikali japo kuna changamoto bado zipo hasa katika suala la usimamizi.

### 4.2.2 Matokeo Yaliyopatikana Kutoka Uwandani (Practical Evidence)

Taarifa za uwandani zililenga (i) kubaini uzingatiaji wa utekelezaji wa Sheria ya Kodi ya Mapato na Kanuni zake za Mwaka 2012 (ii) kutathmini utayari wa wafanyabiashara katika utoaji wa risiti za kielektroniki (iii) kubaini endapo bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea na matumizi ya risiti za kuandikwa kwa mkono, (iv) kuchunguza endapo kwenye uwanda wapo wafanyabiashara wanaotumia risiti halali na zisizo halali na (v) kuchunguza iwapo kuna vitendo vya udanganyifu na rushwa katika matumizi ya mashine za kielektroniki na matokeo ni kama inavyoonekana hapa chini.

i. Kuhusu uzingatiaji wa sheria ya kodi ya mapato, ilibainika kuwa 35% ya wafanyabiashara ndio wanaotumia EFDs. Takwimu zilionesha kuwa tangu kuanza kwa mfumo huo mwaka 2010 wafanyabiashara wanaotumia mashine hizo ni 56967 kati ya wafanyabiashara 152,997. Hii ni sawa na 37% ya lengo la utekelezaji la usajili wa wafanyabiashara kutumia mashine. Aidha, idadi hiyo ya 56967 ni sawa na asilimia 3.8 kati ya idadi ya wafanyabiashara Milioni 1.5 waliotambuliwa na TRA nchi nzima. Tafsiri yake ni kwamba kuna udhaifu katika usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Mapato ya Kodi na Kanuni zake.

ii. Kuhusu utayari wa wafanyabiashara wa kutoa risiti za kielekroniki ilibainika kuwa zaidi ya wafanyabiashara 80% hawapendi matumizi ya risiti za kielektroniki kwa sababu ya: (a)

kutakiwa kulipa kodi kubwa isiyolingana na mitaji yao, (b) kufanyiwa vitendo visivyo vya kiungwana na maofisa wa kodi, (c) huduma duni zisizolingana na kodi zinazolipwa na (d) vitendo vya rushwa. Pia tamaa ya kujipatia faida kubwa kupita kiasi tabia inayochangiwa na wananchi wengi kutokuwa na utamaduni wa kudai risiti mara baada ya kufanya manunuzi. Tafsiri yake ni kuwa Serikali inapaswa kutoa elimu kwa umma wa Watanzania kuhusu faida za kulipa kodi bila kushurutishwa.

iii. Kifungu cha 18 cha Kanuni za Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinaelekeza mazingira ambayo wafanyabiashara wanaweza kuruhusiwa kutumia risiti zilizoandikwa kwa mikono. Mfano, mashine ikiwa na hitilafu na mtumiaji anapaswa kutoa taarifa kwa Kamishna wa Kodi za Ndani (TRA), na vivyo hivyo iwapo mashine inashikiliwa kwa Uchunguzi Maalum au inafanyiwa matengenezo. Ilithibitika kuwa wafanyabiashara wamekuwa wakikwepa kulipa viwango halisi vya kodi kwa kisingizio cha kuruhusiwa kisheria kutumia risiti za mkono wakati sio kweli. Ilibainika kuwa pia baadhi ya wafanyabiashara, wakishirikiana na mawakala na watumishi wa umma hula njama kukwepa kutumia mashine za kielektroniki na hivyo kuikosesha Serikali mapato. Sheria inaelekeza kuwa kabla ya kuanza kutumia risiti zilizoandikwa kwa mkono, mtumiaji anapaswa kuomba kibali TRA. Hata hivyo, ilibainika kuwa 45 % ya wafanyabiashara wamekuwa wakitumia risiti za mikono bila kibali katika maeneo yao ya biashara huku wakiwa na mashine za ‘EFDs’.

iv. Kuhusu uwepo wa karatasi za kughushi, ilithibitika kutoka uwandani kuwa zaidi ya 56% ya wafanyabiashara wamekuwa wakitumia karatasi za kughushi (counterfeit rollers) na kukwepa matumizi ya karatasi halisi zinazopaswa kutumika kisheria. Athari ya kutumia karatasi za kughusi ni pamoja na uharibifu wa mashine na Serikali kukosa mapato inayoyastahili. Pia utafiti ulibaini karatasi hizo zimekuwa zikiuzwa mitaani na wachuuzi bila ya kuwa na hofu ya kukamatwa.

v. Kuhusu uwepo wa vitendo vya rushwa, utafiti ulibaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wanazichezea mashine (temper) kwa makusudi ili zisifanye kazi kwa ufanisi,

wengine wamekuwa na tabia ya kufuta baadhi ya taarifa muhimu zinazotakiwa kwenye risiti au kubadilisha maudhui (content) kwa lengo la kukwepa kulipa kiwango cha kodi stahiki. Mfano, kupunguza idadi ya tarakimu katika kiasi cha fedha kinachotakiwa kukatwa kodi stahiki ya Serikali (total taxable sales). Wafanyabiashara kuandika kiasi kidogo cha fedha ya mauzo ya bidhaa katika risiti tofauti na kiasi halisi cha fedha walichouza. Wafanyabiashara kutumia fursa ya uelewa mdogo wa wateja/wanunuzi kuhusu matumizi ya mashine ya EFD kwa kutotoa risiti za EFD kwa kisingizio cha kutokuwepo kwa mtandao.

### 4.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, Taasisi ilitoa mapendekezo yafuatayo:-

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iongeze juhudi katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kodi za Ndani, Income Tax (Electronic Fiscal Device) Cap.332 na Kanuni zake za 2012 kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu bila kusahau misingi ya uadilifu na weledi.

ii. TRA ichukue hatua za haraka za kudhibiti mianya ya rushwa na vitendo vya rushwa katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na ukwepaji wa Kodi. Hii ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti (internal control mechanisms)

iii. TRA iendelee kutoa elimu kwa umma wote wa Watanzania kuhusu umuhimu wa kulipa kodi bila kushinikizwa kwa ustawi wa Taifa

iv. TRA iimarishe usimamizi wa watendaji wake kwa kufanya ukaguzi wa kawaida na ule wa kushtukiza kwa lengo la kufuatilia uzingatiaji wa matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ikiwemo kudhibiti mienendo ya watumishi wasio waadilifu na pale inapothibitika wanajihusisha na rushwa, kuwachukulia hatua za kisheria.

v. TRA iwe inafanya ukaguzi wa kiufundi (Technical Inspection) wa mara kwa mara wa mashine za kielektroniki ili kupima ubora na uwezo wa mashine hizo kufanya kazi.

vi. TRA ipitie upya mfumo wa Kanzidata wa EFD ili kuhakikisha unakuwa na uwezo wa kurekodi na kutunza taarifa ya mauzo ya kila bidhaa zinazouzwa na wafanyabiashara kwa kutumia mashine hizo.

vii. TRA iwafanyie upekuzi wa kina maafisa waliopewa dhamana ya kukadiria kodi ili kuhakikisha wanazingatia maslahi ya Taifa kwani inaonyesha baadhi yao wanashirikana na wafanyabiashara wasio waaminifu kuikosesha serikali mapato.

### 4.4 Mafanikio na Hitimisho

EFD zikitumiwa vizuri zina uwezo wa kudhibiti vitendo vya rushwa na hivyo kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na makusanyo ya kodi. Aidha, sheria ya Ongezeko la Thamani na Kanuni zake za mwaka 2012, itakuwa na maana tu, pale ambapo itatekelezwa kikamilifu kwa lengo la kuthibiti upotevu wa mapato, kuthibiti vitendo vya udanganyifu na rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watendaji wasio waadilifu kwa maslahi yao binafsi. Aidha, mafaniko ya utekelezaji wa sheria hii yatategemea zaidi ni kwa kiwango gani wananchi na hasa wafanyabiashara wameelimishwa kuhusu faida za kutumika kwa risiti za kieketroniki. Mamlaka ya Mapato inapaswa kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti kwa kuhakikisha kuwa vitendo vyote vya ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma vinabainishwa mapema na hatua stahiki zinachukuliwa kabla ya kutendeka kwa uhalifu. Baada ya tathmini ya TAKUKURU, japo bado changamoto zipo, lakini kumekuwepo na mwitikio chanya wa wafanyabiashara wa kutambua umuhimu wa kulipa kodi bila kushuritishwa na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi. Uongozi wa ‘TRA’ umeahidi kuzifanyia kazi changamoto zote zinazokwamisha ufanisi katika matumizi ya mashine za EFDs nchini. Aidha, ilibainika kuwa tathmini ya Taasisi imeongeza uelewa kuhusu mashine za EFDs na namna zinavyopaswa kutumika kwa ustawi wa Taifa letu.

## 5.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI YA KITAIFA

### 5.1 Utangulizi

TAKUKURU inao wajibu wa kufuatiliaji matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hapa nchini. Wajibu huo unatokana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007, kifungu cha 7(a) na (c) ambayo inaitaka TAKUKURU kutathmini/ kuchambua mifumo mbalimbali ya utoaji huduma ili kubaini mianya ya rushwa na kisha kupendekeza namna bora ya kuiziba. Katika kutekeleza wajibu huo, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 ofisi ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Jumla ya miradi 170 yenye thamani ya shilingi za Kitanzania 1,075,754,558,817.15 ilifuatiliwa. Malengo ya ufuatiliaji huo ilikuwa ni pamoja na kubaini (i) endapo kuna ucheleweshaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi husika (ii) endapo kuna uvujaji wa fedha (iii) endapo thamani halisi ya fedha imepatikana (VFM) (iv) endapo wananchi walishirikishwa katika kupanga na kusimamia utekelezaji wa miradi na (v) changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Kati ya miradi iliyofuatiliwa, jumla ya miradi 162 ilikuwa inatekelezwa katika ngazi za wilaya na mikoa, na miradi 8 ilikuwa ni miradi mikubwa ya kitaifa. Miradi iliyofuatiliwa ni pamoja na (i) Mradi wa kusambaza maji kutoka ziwa Victoria kwenda miji ya Kagongwa-Isaka-Kahama; (ii) Mradi wa kusambaza maji katika miji ya Mugango-Kiabakari-Butiama; (iii) Mradi wa kutoa maji ziwa Victoria kwenda miji ya Tabora, Igunga na Nzega; (iv) Mradi wa Maji safi na Usafi wa Mazingira–Makonde; (v) Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Wanging’ombe; (vi) Mradi wa Maji Chalinze (vii) Mradi wa Maji Same Mwanga Korogwe; (viii) Mradi wa Maji wa Handeni.

Mbinu za ufuatiliaji zilizotumika ni pamoja na ukaguzi wa moja kwa moja miradi husika kutumia orodha ya ukaguzi, mahojiano na majadiliano katika vikundi; kupitia mikataba ya utekelezaji wa miradi; kufuatilia mtiririko wa fedha; kufika maeneo ya mradi na kujionea kazi zilizofanyika kwa

mujibu wa mikataba; kuongea na wananchi wanufaika wa miradi; kufanya mahojiano na viongozi wa Serikali katika ngazi za mikoa, wilaya, kata na vijiji inapotekelezwa miradi; pamoja na Kuhudhuria baadhi ya vikao kazi (site meeting). Aidha, mahojiano yalifanyika yakiwahusisha wasimamizi wa miradi, waratibu wa miradi, wakandarasi, wataalam washauri na baadhi ya watumishi/vibarua waliokuwa katika maeneo inapotekelezwa miradi hiyo.

### 5.2 Matokeo ya Ufuatiliaji

i. Udhaifu katika majadiliano na uandaaji wa mikataba ya kifedha (financing agreement) na ucheleweshaji wa miradi kutokana na Serikali kuchelewa kutoa msamaha wa kodi kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba,

ii. Kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, (iii) urasimu katika utoaji vibali kwa watalaam wa nje wanaotekeleza miradi yenye kuhitaji utalaam hapa nchini,

iii. Kuongezeka kwa gharama kutokana na kubadilika kwa usanifu wa awali wa miradi ya maji,

iv. Ucheleweshaji wa fidia kwa wananchi wanaopitiwa na miradi na hivyo kusababisha wakandarasi kutekeleza miradi kwa vipande vipande,

v. Udhaifu katika ushirikishaji wa Taasisi nyingine katika utekelezaji wa miradi, mfano, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, TAMISEMI, TANESCO, Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Ujenzi na Miundombinu na Wizara ya Ardhi.

vi. Kuhusu miradi mikubwa ya kitaifa ilibainika kuwa (a) kuna udhaifu katika uratibu wa miradi ya maji baina ya Taasisi/Wizara imekuwa ikisababisha miradi ya maji kuchelewa (b) wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati na hivyo kusababisha baadhi ya mikataba kuvunjwa (c) malipo kufanyika kwa kutumia dola za Kimarekani licha ya

miradi kutekelezwa kwa fedha za kitanzania (d) kuweka makadirio ya juu ya gharama za utekelezaji wa miradi kuliko gharama halisi (overly designing) na (e) upotevu wa maji kwa baadhi ya miradi hadi asilimia 70 kutokana na uchakavu wa miundombinu na (e) miradi kushindwa kutekelezwa kwa ubora na kwa wakati.

### 5.3 Mapendekezo

Kufuatia matokeo ya ufuatiliaji huo, Taasisi ilipendekeza mambo yafuatayo:-

i. Upekuzi wa mikataba na makubaliano ya kifedha (financing agreement) ili isikinzane na Sheria za nchi wakati wa utekelezaji wa mikataba na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa utoaji wa vibali vya msamaha wa kodi kwa wakati,
ii. Malipo ya wakandarasi yafanyike kwa wakati ili kuiepusha Serikali kupata hasara inayosababishwa na riba kwa kuchelewa kuwalipa kwa wakati,
iii. Kutekeleza miradi michache ya maji kulingana na kiasi cha fedha kilichopo ili miradi kuikamilisha kwa wakati na ubora;
iv. Kuongeza umakini katika kupitia na kuidhinisha michoro ya kitaalamu (technical drawings) ili iendane na uhalisia wa mazingira halisi ya utekelezaji
v. Kuongeza uhakiki wa vifaa vinavyopokelewa ili kuhakikisha kuwa vinazingatia ubora kwa mujibu wa orodha ya gharama ya vifaa/huduma katika miradi (BOQ)
vi. Kuimarisha usimamizi wa miradi inayotekelezwa na wakandarasi wa ndani na nje ikiwemo kuwawezesha wasimamizi wasaidizi kusimamia utekelezaji wa miradi kwa ukaribu, na
vii. Kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa kwa ajili ya usimamizi wa miradi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa
viii. Kuhamasisha ushiriki wa wadau na Taasisi nyingine za Serikali katika kutekeleza miradi ya maji. Kwa mfano, Wizara ya mambo ya ndani ya Nchi na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya vijana zinapaswa kupunguza urasimu wa kutoa vibali vya kazi na ajira kwa wataalam wa kigeni. Wizara hizi zinapaswa kuweka utaratibu wa kutoa nakala za mikataba kwa viongozi wa ngazi za Mikoa (RAS) na Wilaya (Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa

Halmashauri /Miji na Mamlaka za Maji) ili kuwawezesha viongozi hao kufuatilia na kusimamia miradi ya maji na kuratibu ulipaji fidia kwa wananchi wanalazimika kupisha utelekezaji wa miradi ya maji.

### 5.4 Mafanikio na Hitimisho

Kufuatia ufuatiliaji wa miradi ya maji, matokeo yaliwasilishwa kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kupitia majadiliano ya vikao kazi na kushauri maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi. Jambo la kutia moyo ni kwamba Wizara yenye dhamana imeanza kutekeleza baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Taasisi kwa minajili ya kuziba mianya ya rushwa na kuhakikisha kuwa miradi ya maji inatekelezwa kwa ubora na thamani haisi ya fedha inapatikana. Aidha, kwa maeneo ambayo yalihitaji uchunguzi, Taasisi imeanzisha uchunguzi wa tuhuma za rushwa. Pia utoaji wa elimu kwa umma unaendelea kwa kuwahimisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maji na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa Taasisi. Mwisho, wizara yenye dhamana kwa kushirikiana na wadau, imeahidi kuchukua hatua kurekebisha dosari zilizoainishwa na ufuatiliaji uliofanywa na TAKUKURU ili thamani ya fedha ipatikane.

# 6.0 RUSHWA KATIKA MFUMO WA UHAULISHAJI AWAMU III WA TASAF

## 6.1 Utangulizi

Tangu tupate uhuru mwaka 1961 imekuwa ikipambana na maadui wakuu watatu ambao ni Ujinga, Umaskini na Maradhi. Juhudi za serikali katika kupambana na maadui hawa zimekuwa zikifanyika kwa kuandaa sera, mikakati na mipango ya maendeleo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi. Kufuatia sera na mikakati hiyo, tafiti zinaonesha hali ya umaskini imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka katika miaka ishirini iliyopita, lakini maendeleo yamekuwa ni yenye kutofautiana kati ya mtu na mtu, kati ya jamii moja na nyingine, kati ya sehemu moja na nyingine.

Sera na mikakati ya Serikali kama Mkakati wa kutokomeza umaskini Tanzania (MKUKUTA), Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania (MKUKUTA), Mpango wa kati wa matumizi (Medium Term Expenditure-MTEF), Kilimo Kwanza na Mapinduzi ya kijani, na Dira ya maendeleo 2025 ni baadhi ya sera na mipango iliyoanzishwa ili kupunguza umaskini. Mipango na sera hizi zimekuwa zikileta matokeo chanya katika maendeleo kwa kuimarisha elimu, afya na miundombinu ya barabara ili kuyafikia maendeleo endelevu. Pamoja na mchango wa sera na mikakati hii, bado jamii maskini imekuwa ikibaki nyuma kimaendeleo na kuendelea kuwa maskini  wa kipato cha ndani cha kaya ikiwa ni pamoja na uwezo wa kupata chakula. Pia hadi kufikia mwaka 2000, nusu ya watanzania walikuwa ni maskini ambapo inakadiriwa kuwa moja ya tatu ya watanzania wanaishi katika umaskini wa kupindukia (TASAF, 2013). Hali hii ilisababisha Serikali  kuingilia kati kwa kuja na mkakati wa kuwainua maskini ili nao waweze kushiriki katika maendeleo ya nchi yao kwa kuwa na kipato cha kuweza kugharamia mahitaji yao ya kila siku na kujiengua katika athari zinazosababishwa na umaskini wa kupindukia (Ibid, 2013).

### 6.2 Utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Tatu (TASAF III)

Mkoa wa Simiyu ni moja ya mikoa ambayo wilaya zake zinatekeleza mpango huu wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii awamu ya tatu (TASAF III). Katika wilaya zake zote tano za Itilima, Bariadi Vijijini na Bariadi Mji, Meatu Maswa Busega mpango huu ulitekelezwa katika vijiji 329 vyenye kaya 41,575 zilizosajiliwa.katika dirisha la uhaulishaji la mwezi Aprili, 2018 na jumla ya kaya 4,042 ziliondolewa na kubaki na walengwa 37,533 kwa mkoa. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013 hadi sasa, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) unapoendelea kutekeleza malengo yake ya awamu ya tatu ya kukabiliana na umaskini kupitia mpango wake wa kuzisaidia kaya maskini kutoka kwenye umaskini kupata kipato chenye kuwawezesha kukidhi mahitaji yao. Wakati Mfuko unaendelea kuongeza nguvu ya kuziinua kaya maskini kiuchumi, jamii imeshuhudia mapinduzi ya kipato na kuinuka kwa kaya maskini zilizo chini ya mpango huu. Mfuko pia umeleta mapinduzi chanya ya kipato kwa wanufaika; umewafanya wanufaika kuweza kujenga nyumba za kisasa, kusomesha watoto wao, kupata lishe bora, kufungua biashara, kuanzisha miradi ya ufugaji na kilimo cha kisasa, na kuwaunganisha wananchi katika vikundi vya uzalishaji na biashara ndogondogo na kuboresha hali za maisha yao na hasa kiuchumi.

### 6.3 Matokeo ya Ufuatiliaji

Kufuatia ufuatiliaji uliofanywa na ofisi ya TAKUKURU Simiyu kuanzia mwezi Agosti, hadi Disemba, 2017; ilibainika kuwa kaya maskini na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zimekuwa zikipokea fedha za kunusuru kaya maskini kutoka TASAF kila baada ya miezi miwili.

i. Imebainika kuwa asilimia kubwa (99.9%) ya wapokeaji ni walengwa wa mradi na wanufaika wa fedha za TASAF ambao wamekuwa wakihama kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Cha kushangaza ni kwamba fedha zimeendelea kuletwa kutokana na uzembe wa Kamati za Ufuatiliaji na Waratibu wa TASAF kwa kushindwa kuchukua hatua mapema na kujihusisha na vitendo vya rushwa. Mfano, ufuatiliaji ulibaini uwepo wa wanufaika 28 ambao hawakulipwa lakini fedha TAS 1,204,500 hazijarejeshwa. Pia ilibainika kuwa wanufaika

wanapofariki hawaondolewi kwenye mpango huo wa malipo na hivyo ndugu au jamaa hutumia vitambulisho vya marehemu kuchukua fedha wakiwemo viongozi wa vijiji na kata kwa kutumia vitambulisho vya watu ambao hawako hai. Vilevile ufuatiliaji ulibaini uwepo wa manunuzi ya jumla Tsh.11, 967,113.50 yamefanywa kwa fedha za TASAF pasipo stakabadhi za kielektronini (EFD receipts), na matumizi ya fedha za kununua mafuta kiasi cha Tsh.13,045,402.50 pasipo kuwepo na nyaraka za kuthibitisha matumizi ya mafuta lita 6,689.9 (logbook za magari yaliyotumia mafuta hayo) kwa muda wa miezi mitatu.

### 6.4 Mapendekezo

Kufuatia matokeo ya ufuatiliaji huu, Taasisi ilipendekeza yafuatayo ili kuziba mianya ya rushwa

i. Watendaji na viongozi wanaohusika na mpango wa uhaulishaji kupitia fedha za TASAF kuzingatia miongozo na mikataba baina ya TASAF na Halmashauri;
ii. Kufanya uhakiki wa orodha ya wanufaika kila mwezi ikiwemo kuchukua hatua za haraka pale inapotokea baadhi ya wanufaika wamehama au wamefariki;
iii. Kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya fedha kwa wanufaika kwa kuwakumbusha umuhimu wa kuwekeza kwenye uzalishaji; na kuwachukulia hatua wale wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa bila hofu wala upendeleo
iv. Kujenga utamaduni wa kufanya malipo au manunuzi yote kwa kutumia mashine za EFD;
v. Kufanya uhakiki wa kina ili watu wenye uwezo kiuchumi waondolewe na kuandikisha kaya maskini zisizojiweza kiuchumi. Hii ni pamoja na kuwaondoa viongozi wote kwenye orodha ya wanufaika.

### 6.5 Mafanikio na Hitimisho

Ufuatiliaji wa fedha za uhaulishaji kupitia TASAF III unaotekelezwa katika wilaya tano za Itilima, Bariadi Vijijini na Bariadi Mji, Meatu Maswa Busega umebaini uwepo wa mianya ya rushwa na kutoa mapendekezo kwa halmashauri ya Simiyu kuchukua hatua za haraka kuziba

mianya hiyo. Pamoja na kuwepo kwa changamoto za kiuongozi, ufuatiliaji huu umekuwa ukitekelezwa kwa mafanikio katika vijiji 329 vyenye kaya 41,575 zilizosajiriwa. Mfano, ilibainika kuwa katika dirisha la uhaulishaji la mwezi Aprili, 2018, jumla ya kaya 4,042 ziliondolewa na kubaki na walengwa 37,533 kwa mkoa. Pia ufuatiliaji wa Taasisi umesaidia kuwakumbusha waratibu na viongozi wanaosimamia mpango huu kuhusu masuala ya usimamizi ya miradi na fedha. Aidha, kutokana na ufuatiliaji wa Taasisi, kumekuwepo na matumizi ya fedha yanayozingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha za umma. Matokeo yake ni kwamba mpango umeweza kutoa ajira za muda mfupi kwa walengwa, kuanzisha wa miradi ya maendeleo ikiwemo uchimbaji wa visima, kukarabati wa mabwawa, kujenga nyumba za kisasa kwa walengwana na kusomesha watoto. Faida nyingine ya ufuatiliaji huu ni wananchi kuanza kupata lishe bora, kufungua biashara, kuanzisha miradi ya ufugaji na kilimo cha kisasa na biashara ndogondogo. Mwisho, ilibainika kuwa kutokana na ufuatiliaji wa Taasisi, mpango huu umeweza kuwaunganisha wananchi katika vikundi vya uzalishaji na zaidi 95% ya wapokeaji/walengwa wamekuwa wakinufaika na mradi wa TASAF III.

# 7.0 RUSHWA KATIKA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA CHAMA CHA USHIRIKA CHA KINYAKI

## 7.1 Utangulizi

Ushirika ni moja ya nguzo muhimu za kiuchumi zenye uwezo wa kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini na kati kuanzisha na kumiliki chombo chao (chama cha ushirika). Ushirika unaweza kuchangia mtaji unaohitajika kwa usawa na wanachama kukubali kuyakabili matatizo yao kiuchumi kwa kutumia fedha na mitaji wanazochangia. Ushirika pia unatoa fursa kwa wananchi wa makundi mbalimbali kuunganisha nguvu zao katika kujijengea uwezo wa kifedha ambao ni muhimu katika kukabiliana na mahitaji ya kila siku. Katika vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa, wanachama wana jukumu la kutatua matatizo yao ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia juhudi zao za pamoja katika kufikia malengo ambayo yasingefikiwa kwa urahisi kwa juhudi za mtu mmoja mmoja.

Kutokana na dhana ya umoja ni nguvu, ushirika hukusanya fedha kutoka kwa watu waliojiunga kwa hiari na kukubaliana kuweka fedha zao pamoja na kisha kukopeshana kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi na kijamii. Wanachama wa ushirika wa kuweka na kukopa huwa na fungamano la pamoja. Fungamano hilo linaweza kuwa eneo wanaloishi, kuajiriwa na mwajiri mmoja, kuwa na ajira zinazofanana (kama vile walimu katika wilaya ya Meatu), kusali katika msikiti, kanisa na au dhehebu au dini moja  Aidha, chama cha ushirika cha kuweka na kukopa cha walimu wa wilaya ya Meatu kilianzishwa mwaka 2000 kwa jina la Kinyaki Teachers Savings and Credit Cooperative Society Ltd. Iikiwa Kinyaki ni kifupi cha majina ya Tarafa 3 za wilaya ya Meatu ambazo ni Kimali, Nyalanja na Kisesa. Chama hiki cha ushirika wa kuweka na kukopa kilipewa usajili na Msajili wa vyama vya ushirika kwa namba ya usajili SHR 1019. Chama hiki cha ushirika kiliundwa na walimu wanaofanya kazi katika Halmashauri ya wilaya ya Meatu kwa lengo la kuchangia mtaji ili kuyakabili matatizo ya kiuchumi na kijamii. Kinyaki inatekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015. Pamoja na

kuwepo kwa sheria, kanuni na sera zinazoelekeza namna bora ya utendaji wa chama cha ushirika, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo ubadhirifu wa mali na vitendo vya rushwa. Kwa sababu hiyo, Taasisi ya Kuzuia na Kupamabana na Rushwa (TAKUKURU) wilaya ya Meatu iliona kuna haja ya kufanya ufuatiliaji wa mianya ya rushwa kwa mujibu wa kifungu cha 7(a) na (c) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 na kisha kushauri namna bora ya kuiziba mianya hiyo. Ufuatiliaji ulifanyika kuanzia mwezi Februari –Machi 2018 kwa lengo la: (i) kubaini upotevu wa mapato katika uendeshaji wa chama cha ushirika cha Kinyaki (ii) kubaini madhara yaliyosababishwa na ubadhirifu wa fedha kwa chama cha ushirika Kinyaki (iii) kupendekeza namna ya kuzuia mianya ya rushwa.

### 7.2 Matokeo ya Ufuatiliaji

Ufuatiliaji huo ulibaini mambo yafuatayo:-

i. Kutokuwepo kwa mfumo mathubuti wa udhibiti wa ndani (weak internal controls)
ii. Tabia iliyokubuhu ya baadhi ya wana-ushirika kujilipa ‘malipo hewa’
iii. Baadhi ya mali za ushirika kutokuorodheshwa kwenye daftari la mali za ushirika
iv. Baadhi ya malipo kufanyika pasipokuwa na maelekezo/kibali na;
v. Michango ya wanachama kutowasilishwa kwa wakati bila kuwa na maelezo yakuridhisha.

### 7.3 Mapendekezo

Kufuatia matokeo ya ufuatiliaji huo, Taasisi ilipendekeza yafuatayo kuziba mianya ya rushwa

i. Kuhusu tatizo la malipo hewa, ilipendekezwa kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti ya ndani sanjari na kufanya uchunguzi wa kuwabaini wale wote waliohusika na kisha kuchukua hatua zinazofaa;
ii. Kuhusu tatizo la kutokuwaepo kwa viwango maalumu vya malipo ya fedha, ilipendekezwa Chama cha Kinyaki kuanzisha Kanuni za Fedha na Miongozo itakayosimamia malipo ya posho kwa wanachama waliajiriwa na chama.

Kanuni/miongozo hiyo inapaswa kufahamika kwa wanachama wote na kuzingatiwa;

iii. Kuhusu tatizo la kutoorodhesha baadhi ya mali za chama kwenye rejista maalum, ilipendekezwa uanzishwaji wa rejista maalum kwa ajili ya kuzitambua mali zote za chama na kuzitunza kwa utaratibu mzuri;

iv. Kuhusu baadhi ya malipo kufanyika pasipo kuwa na maelezo yanayojitosheleza, ilipendekezwa kuwa kuanzia sasa malipo yote *LAZIMA* yaambatane na uhalali/sababu ya kuyalipa, vinginevyo yoyote atakayehusika kufanya malipo bila kuwa na uhalali (justification) atachukuliwa hatua za kinidhamu

v. Kuhusu ununuzi wa vifaa, ilipendekezwa kuwa manunuzi yote ya vifaa yaorodheshwe kwenye daftari la kupokelea vifaa (Store control Book) . Pia Uongozi uhakikishe chama kinakuwa na vitabu vyote muhimu vya fedha na vifaa ili kuwa na usahihi wa taarifa juu ya fedha na vifaa

### 7.4 Mafanikio na Hitimisho

Baada ya ufuatiliaji uliofanywa na TAKUKURU katika chama cha ushirika cha Kinyaki matokeo yaliwasilishwa kwa mamlaka husika na hatua mbalimbali kuchukuliwa kwa lengo la kuimarisha chama ili wanachama waendelee kuwa na imani na chama chao. Mrejesho tunaoupata ni kwamba karibu mapendekezo yote yaliyotolewa na Taasisi yanaendelea kufanyiwa kazi na Uongozi wa chama umeahidi kuendelea kuyatekeleza ili kuhakikisha kuwa maeneo yenye dosari (rushwa) yanapatiwa ufumbuzi. Tangu ufuatiliaji huu ufanyike hakuna malipo yanayofanyika bila kuwa na maelezo/uhalali wa kuyalipa. Pia uongozi wa chama umekwisha andaa rasimu ya kanuni za fedha tayari kwa kuiwasilisha kwenye kikao cha wanachama na Kamati ya Usimamizi (KU) kwa ajili kujadiliwa na kupitishwa. Uongozi wa chama umeanza kuorodhesha mali za chama kama ilivyopendekezwa. Lengo la hatua hizi ni kuhakikisha kuwa rasilimali za chama zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Haya ni baadhi ya mafanikio yalliyotokana na ufuatiliaji.

# 8.0 UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA AFYA NGARA

## 8.1 Utangulizi

TAKUKURU wilaya ya Ngara ilifanya ufuatiliaji miradi ya maendeleo kwenye sekta ya Afya kwa vile inatoa huduma muhimu katika maisha ya kila mwananchi. Inakadiriwa kuwa asilimia 80 ya wakazi wapatao milioni 34 nchini wanaishi vijijini, pamoja na upungufu mkubwa wa huduma za afya, Serikali imekua ikifanya jitihada za kuhakikisha kuwa wananchiwanapata huduma bora. Mwaka 2018 Benki ya Dunia (WB) ilitoa fedha Tsh 800,000,000/= (shilling milioni mia nane) kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya Afya vya Murusagamba na Mabawe katika wilaya ya Ngara katika Mkoa wa Kagera. Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha hizo ili kuona iwapo zimetumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwamba thamani halisi ya fedha (VFM) imepatikana. Madhumuni mahsusi ilikuwa ni pamoja na kuchunguza namna fedha za umma zinavyotolewa, njia zinazopitia, zinavyopokelewa katika ngazi na zinavyotumika. Pia ulilenga kugagua namna miradi ilivyotekelezwa na kuchunguza endapo thamani halisi ya fedha imepatikana na hivyo kudhibiti vitendo vya rushwa. Haya ndiyo yalikuwa malengo ya ufuatiliaji.

## 8.2 Hali ya Mradi Wakati wa Ufuatilaji

Katika kituo cha Afya cha Murusagamba ujenzi uliotekelezwa ulikuwa ni ujenzi wa Nyumba ya Daktari Mfawidhi, Ukamilishaji wa Ujenzi wa jengo la Upasuaji (Theatre), jengo la wagonjwa wa Nje (OPD), Jengo la wagonjwa wa Ndani (IPD) na Jengo la sehemu ya kufulia (Laundry).



Picha Na. 1: Jengo la Wodi ya OPD, Kituo cha Afya-Murusagamba Wakati wa Ufuatiliaji

Kituo cha Afya cha Mabawe kulikuwa na ujenzi wa Jengo la Upasuaji (Theatre), Jengo la wagonjwa wa ndani (IPD Ward), Nyumba ya Daktari Mfawidhi (Nyumba ya mtumishi). Ujenzi huu ulifanyika kwa kutumia utaratibu wa "Force Account" kujenga pasipo kutumia wakandarasi.



Picha Na. 2: Jengo la Sehemu ya Upasuaji, Kituo cha Afya-Mabawe Wakati wa Ufuatiliaji

### 8.3 Matokeo ya Ufuatiliaji

Ufuatiliaji ulibaini mambo yafuatayo:-

i. Ilibainika kuwa ujenzi wa vituo hivyo vya afya havikuweza kukamilika kwa wakati kutokana na kucheleweshwa kwa fedha za ujenzi kutoka kwenye Wizara yenye dhamana. Mfano mnamo mwezi Disemba, 2017 Wizara ya Afya ilituma fedha Tsh 800,000,000/= (milioni mia nane) kwenye akaunti ya Idara ya Afya ya Halmashauri na baada ya mwezi mmoja yaani Januari 2018, fedha kiasi cha Tsh 400,000,000/= ndio kilipelekwa kwenye akaunti ya kituo cha Afya cha Murusagamba na Tsh 400,000,000/= kwenye akaunti ya kituo cha Afya cha Mabawe.
ii. Ufuatiliaji ulibaini ushirikishwaji mdogo wa Wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa miradi hiyo. Ilibainika kuwa wajumbe wengi walikuwa hawajui majukumu yao na hivyo kutumia muda mwingi kuhudhuria vikao kama watazamaji (onlookers)
iii. Uwepo wa makadirio ya juu ya gharama za ujenzi na ufundi kuliko bei halisi iliyoko sokoni (over-estimation);
iv. Mwongozo wa ujenzi kutoeleza kwa ufasaha majukumu ya kila mdau katika ujenzi huo. Mfano mwongozo hausemi nani mwenye jukumu la kutoa zabuni kwa aliyeshinda kati ya Mkurugenzi Mtendaji au Mganga Mfawidhi wa Kituo cha afya

### 8.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya ufuatiliaji huu, yafuatayo yalipendekezwa kuziba mianya ya rushwa

i. Halmashauri iwe inatoa taarifa za fedha mapema iwezekanavyo kwenye idara husika (user department) kuhusu uwepo wa fedha ili ziweze kuombwa kwa wakati na kuanza utekelezaji wa mkiradi bila kuchelewa. Ilipendekezwa angalau muda wa wiki mmoja tangu zifike kwa 'DED' fedha hizo zihamishwe kwenda kwenye idara inayohusika
ii. Baadhi ya miradi haitekelezwi kwa ubora kwa sababu ya shinikizo la kisiasa. Mfano Mwenge au Ziara za viongozi zimekuwa zikitumika kama kichaka cha baadhi ya wasimamizi kufanya matumizi yasiyo na kibali au kufuja fedha kwa kusingizia ugeni wa viongozi wa kitaifa au mwenge. Uharaka huu umesababisha taratibu za fedha

kutokufuatwa na baadhi ya watumishi wasio waadilifu kutumia mwanya huo kufuja fedha za umma.

iii. Uandaaji wa nyaraka za mkataba na ramani ufanyike mapema ili kupunguze mabadiliko ya mara kwa mara katika miradi ili kuwabana mafundi kuongeza gharama zisizo za lazima

iv. Tathmini ya vifaa pamoja na gharama za ujenzi zifanyike kwa umakini na kwa ulinganisho wa bei ya soko kudhibiti watendaji wasio waadilifu kujiongezea bei isiyolingana na uhalisia wa bei za soko.

### 8.5 Mafanikio na Hitimisho

Ufuatiliaji wa ujenzi wa vituo vya afya vya Murusagamba na Mabawe katika Wilaya ya Ngara ulifanyika kwa lengo la kukagua endapo matumizi ya fedha kiasi cha TAS 800,000,000/= zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwamba thamani halisi ya fedha imepatikana. Taasisi iliwasilisha matokeo haya kwenye uongozi wa halmashauri ya Ngara na kujadiliana kwa pamoja; ili kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa katika ujenzi wa vituo vya afya na miradi mingine inayotekelezwa wilayani humo. Baada ya hatua za Taasisi, mrejesho uliopatikana ni kwamba Mkurugenzi Mtendaji na Timu ya wayendaji wengine wamekubali kurekebisha dosari ambazo ufuatiliaji uliofanywa na Taasisi uliziainisha. Aidha, Uongozi wa halmashauri ya Ngara umeahidi kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika kuhakikisha kuwa miradi yote wilayani humo inatekelezwa kwa ubora na ndani ya wakati na hivyo kudhibiti vitendo vya rushwa. Halmashauri imeahidi kutenga fedha kwa ajili ya kuwapeleka watumishi wake kuhudhuria mafunzo ya usimamizi wa miradi na fedha (project management) jambo ambalo litasaidia kujenga uwezo wa ndani wa halmashauri wa kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo.

# 9.0 THAMANI YA FEDHA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA INAYOSIMAMIWA NA TARURA WILAYANI LINDI

## 9.1 Utangulizi

Wakala wa Taifa wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Road Agency - TARURA) ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali namba 211 la mwaka 2017 na Wakala kuanza kufanya kazi rasmi Mwezi Julai 2017. TARURA Halmashauri ya Wilaya ya LINDI katika mwaka wa 2017/18 ilipokea fedha Tsh. 871,881,415.27 hadi kufikia tarehe 17/05/2018. Katika Bajeti ya fedha za Mfuko wa Barabara, TARURA Wilaya ya LINDI iliomba Tsh. 530,530,000/= ili kukarabati maeneo korofi na kufanya matengenezo kama ifuatavyo: Barabara za Madangwa – Nachunyu – Shuka Tsh. 141,160,000/=, Chikonji – Nangaru Tsh. 111,370,000/=, Mnolela – Simana - Nampunga Tsh. 67,400,000/=, Kitomanga – MvuleniTsh. 72,390,000/= na Mkwajuni – Namkongo Tsh. 105,980,000/=. Katika fedha hizo zote, kiasi cha Tsh. 530,530,000/= kilikuwa kimetolewa hadi kufikia tarehe 17/05/2018. TARURA Mkoa wa LINDI iliingia Mikataba na Makampuni mbalimbali kwa ajili ya kukarabati barabara hizo kulingana na makisio ya fedha walizoomba katika Bajeti ya mwaka 2017/18. Katika utekelezaji huo, Uongozi wa Mkoa uliingia mkataba wa Tsh 178, 740, 854/= na kampuni ya Chaste Investment Ltd kutengeneza barabara za Madangwa – Nachunyu – Shuka na Mnolela – Simana – Nampunga. Mkataba huo ulikuwa ni wa miezi 4 kuanzia tarehe 28/02/2018 hadi tarehe 28/06/2018. Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa LINDI iliona iko haja ya kufuatilia ukarabati wa barabara mbili za Madangwa – Nachunyu – Shuka na Mnolela – Simana - Nampunga ambazo thamani yake ilikuwa ni kiasi cha Tsh. 208,560,000/= kati ya Barabara hizo tano za wilaya hiyo. Lengo la ufuatiliaji lilikuwa ni kutathmini uzingatiaji wa thamani halisi ya fedha (Value for Money tracking) katika utekelezaji wa miradi ya barabara zinazosimamiwa na TARURA. Ufuatiliaji umefanyika katika kipindi cha Mwezi mmoja kuanzia Mei hadi Juni 2018, Eneo la ufuatiliaji ni eneo la ukarabati wa Barabara za Madangwa – Nachunyu – Shuka na Mnolela – Simana – Nampunga kwenye vijiji husika katika halmashauri ya wilaya ya Lindi.

### 9.2 Matokeo ya Ufuatiliaji

Matokeo ya ufuatiliaji huo ni kama ifuatavyo:-

i. Ufuatiliaji ulibaini kuwepo kwa uzingatiaji wa thamani ya fedha katika utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa maeneo korofi na matengenezo ya barabara za Madangwa – Nachunyu – Shuka na Mnolela – Simana – Nampunga. Fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko wa Barabara hadi tarehe 27/06/2018 zilifanyiwa ukaguzi na ilibainika kuwa kiasi cha Tsh. 51,276,900 kilikuwa tayari kimelipwa kulingana na cheti cha malipo namba 1. Hii ni Asilimia 29 ya mkataba wa Tsh. 178,740,854/=.
ii. Ufuatiliaji huu ulibaini kuwa mkandarasi amechelewa kukamilisha kazi kwa wakati kinyume na makubaliano ya mkataba. Mkataba ulielekeza kuwa ifikapo tarehe 28/8/2018 ukarabati wa barabara za Madangwa – Nachunyu – Shuka na Mnolela – Simana – Nampunga ziwe zimekamilika. Hata hivyo, kufikia tarehe 27/06/2018 kazi ya ukarabati iikuwa imetekelezwa kwa asilimia 29 tu ya mkataba. Aidha, uongozi wa TARURA mkoa wa LINDI ulieleza kuwa mkandarasi aliomba kuongezewa muda wa mwezi mmoja hadi tarehe 27/07/2018 kutokana na kucheleweshwa na mvua na maombi yake yalikubaliwa.
iii. Ufuatiliaji ulibaini kuwepo kwa tofauti ya vipimo katika baadhi ya maeneo yaliyokwisha fanyiwa ukarabati. Pia ilibainika kuna tofauti ya vipimo katika ujenzi wa mitaro ya kutolea maji. Katika mahojiano na meneja wa mradi na mkandarasi ilikubalika kuwa maeneo yote yenye upungufu yafanyiwe marekebisho na mkandarasi.

### 9.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya ufuatiliaji huo, yafuatayo yalipendekezwa ili kuziba mianya ya rushwa

i. Meneja wa TARURA wilaya ya Lindi ahakikishe kuwa wakandarasi wanatekeleza kazi yao kwa wakati kuepusha Serikali kuingia harasa kwa kulipa zaidi kutokana na muda wa kutekeleza mradi kuwa mrefu kinyume na masharti ya mkataba;
ii. Meneja wa TARURA Wilaya ya Lindi ahakikishe kuwa mkandarasi anafanya marekebisho ya vipimo kwenye maeneo yote yaliyobainika kuwa na mapungufu

iii. Meneja wa TARURA ahakikishe kuwa marekebisho yanayofanyika kila mwaka ya barabara za vumbi yahusishe pia umwagaji wa kifusi na kushindilia maeneo korofi ili barabara ziweze kudumu.

### 9.4 Mafanikio na Hitimisho

Lengo la ufuatiliaji huu ililikuwa ni kutathmini endapo ukarabati wa barabara mbili za wilaya ya kati ya tano zimekarabatiwa kwa ubora na thamani ya fedha imepatikana. Ufuatiliaji wa Taasisi ulibaini dosari kadhaa utekelezaji wa kazi hiyo. Dosari hizo ni pamoja na kuchelewa kukamilisha kazi kwa wakati, na kutofautiana kwa vipimo kwenye maeneo ambayo ukarabati ulikuwa umekamilika. Hata hivyo, baada ya muda wa utelekelezaji kumalizika, Taasisi ilifanya ufuatiliaji mnamo tarehe 11 mwezi Novemba 2018 na kubaini kuwa ukarabati ulikamilika tangu mwezi Septemba 2018, na mkandarasi alikuwa amefanya marekebisho yote kama alivyokuwa ameelekezwa. Huu ni ushahidi kuwa wakandarasi wakisimamiwa vizuri, thamani ya fedha itapatikana. Ni matarajio ya TAKUKURU kuwa watendaji/viongozi wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini, watatekeleza wajibu wao ipasavyo kwa kuhakikisha kuwa hakuna fedha inayopotea bure na kwamba vitendo vya rushwa vinadhibitiwa.

# 10.0 MATUMIZI YA ‘FORCE ACCOUNT’ KATIKA UJENZI WA KITUO CHA AFYA MNAZI MMOJA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

## 10.1 Utangulizi

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wadau wa Maendeleo waliandaa Mpango Mkakati wa Taifa wa Pamoja (II) wa kupunguza Vifo vya kina Mama na Watoto (2016 - 2020). Hii ilitokana na takwimu kuonyesha hadi kufikia mwaka 2016 vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 556 kati ya watoto 100,000. Mpango huu umelenga kuboresha Huduma za Afya za Ngazi ya Msingi ambako ndiko walipo wananchi na kupunguza idadi ya vifo hadi kufikia 292,100,000 mwaka 2020. Mfumo wa utoaji huduma za Afya nchini ni wa rufaa ikiwa na maana huduma za Afya zinaanzia ngazi ya Msingi katika Zahanati na Vituo vya Afya, ikifuatiwa na Hospitali za Wilaya na Mkoa (Secondari Health Care) na mwisho Hospitali za Kanda za Taifa (Tertiary Health Care). Huduma ngazi ya Msingi na Sekondari zinasimamiwa na TAMISEMI wakati Ngazi ya Taifa zinasimamiwa na Wizara ya Afya. Kati ya Vituo vya Afya 513 vilivyopo sasa ni vituo 115 tu ndivyo vinatoa Huduma za dharura na upasuaji kwa kina mama. Mpango Mkakati huu unalenga kuboresha huduma za Afya ya Msingi ili kukarabati na kujenga vituo vya afya vipya 592 hadi kufikia 2020 vitakavyotoa huduma ya dharura na upasuaji.

Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika mwaka wa fedha 2017/18 imetuma fedha takribani 59 bilioni kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya ambapo Halmashauri ya Manispaa ya LINDI imetumiwa Tsh. 400,000,000/= kutoka Serikalini, Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 700,000,000/= kwa ajili ya kukarabati na kujenga kituo cha afya cha Mnazi Mmoja. Katika mwongozo wa matumizi ya fedha hizo, Katibu Mkuu TAMISEMI ameelekeza kuwa ukarabati na ujenzi ufanyike kwa utaratibu wa “Force Account” kama kifungu namba 167 cha Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 kinavyoelekeza. Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa LINDI ilifanya ufuatiliaji wa mradi huo. Lengo

la ufuatiliaji huo lilikuwa ni kuchunguza endapo wasimamizi wa miradi ya maendeleo wanazingatia matumizi sahihi ya 'force account'.

### 10.2 Matokeo ya Ufuatiliaji

Ufuatiliaji huu ulibaini mambo yafuatayo:-

i. Kwa ujumla ilibainika kuwa ukarabati na ujenzi ulizingatia masharti na matumizi sahihi ya utaratibu wa 'force account' 60% katika ujenzi wa kituo cha afya Mnazi Mmoja katika Manispaa ya LINDI. Hii ni kwa sababu ujenzi uliofanywa na mafundi wenyeji/wazawa na kusimamiwa na Mhandisi wa Manispaa ya LINDI kujenga majengo 10 hadi kufikia hatua ya kuezeka. Hata hivyo, ufuatiliaji ulibaini dosari kwa vile taratibu za manunuzi kukiukwa kununua baadhi ya vifaa bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma. Ilibainika kuwa malipo yalifanyika bila vifaa vya ujenzi kupokelewa

ii. Ufuatiliaji huu ulibaini kuwa fedha za ujenzi wa kituo cha afya Mnazi Mmoja kiasi cha Tsh. 700,000,000/= mara baada ya kupokelewa na Halmashauri ya Manispaa ya LINDI kilihamishwa katika akaunti ya zahanati ya Mingoyo iliyopo Mnazi Mmoja mnamo tarehe 25/01/2017. Fedha hizo zilitanguliwa na michoro na nukuu za bei (BOQ) za majengo yote yaliyopaswa kujengwa na kufanyiwa ukarabati kwa kutumia fedha hizo.

iii. Ufuatiliaji huu ulibaini kuwa Kamati za Usimamizi (KU) ya Manispaa na Kijiji zilitoa tangazo la kutafuta mafundi wenye sifa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kituo cha afya Mnazi Mmoja mkoani Lindi.Katika mchakato huo, mafundi kumi (10) waliomba kazi ya ujenzi wa kituo cha afya na kufanyiwa tathmini na Kamati hizo mnamo tarehe 31.01.2018. Pia mafundi sita (6) walipitishwa baada ya kufanyiwa usaili japo baadaye fundi mmoja kwa sababu anazozijua mwenyewe aliamua kujitoa na kubaki watano waliopewa kazi hiyo.

iv. Ufuatiliaji huu ulibaini kuwa maelekezo ya barua ya Katibu Mkuu- TAMISEMI kufuatwa kwa matumizi ya taratibu za ununuzi wa moja kwa moja (Single Source), ushindanishi wa bei (Competition) na nukuu za bei (Quotation) kutumika katika Manunuzi ya vifaa vya Ujenzi. Katika mahojiano na Kamati za Usimamizi wa mradi ilielezwa kuwa utaratibu huu ulisaidia kupatikana kwa saruji kutoka kwa wakala wa kiwanda cha saruji cha DANGOTE Mtwara kwa

bei ya Tsh. 10,600/= kwa Mfuko wa Saruji 32.5 badala ya Tsh 15,000 bei ya sokoni Lindi mjini. Hali kadhalika mabati yalinunuliwa kwa kufuata utaratibu huohuo.

v. Ufuatiliaji huu ulibaini wajumbe wa Kamati ya Usimamizi (KU) ya kijiji kutoshirikishwa katika kufanya manunuzi. Katika mahojiano, wajumbe wa Kamati hiyo walieleza kuwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi hufanyika bila ya wajumbe kushirikishwa kwa sababu viongozi wa nagazi ya mkoa hutoa maelekezo ya moja kwa moja ya nini kifanyike.

vi. Ufuatiliaji ulibaini kuwa mafundi hulipwa fedha bila kuwepo kwa taarifa ya ukaguzi kutoka kwa Mhandisi wa Manispaa kinyume na taratibu zinazoelekeza kuwa kabla ya malipo kufanyika kwa wakandarasi, taarifa ya ukaguzi ni muhimu ili kuthibitisha ubora wa kazi iliyofanyika.

vii. Pia ufuatiliaji ulibaini kuwa baadhi ya malipo yaliyofanywa kwa wazabuni waliotoa huduma bila kupokelewa kwa bidhaa au vifaa kinyume na K/F 59 cha Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa za mwaka 2010 inayoelekeza bidhaa iliyonunuliwa kukaguliwa kwanza na mtaalamu kabla ya kuingizwa kwenye kitabu cha stoo (store ledger).

viii. Ufuatiliaji ulibaini kuwa kati ya tarehe 26/02/2018 hadi 25/04/2018 fedha kiasi cha Tsh. 35,216,660/= zililipwa kwa mzabuni 'CHANGJIANG INVESTMENT Ltd' iliyopo Mtwara kwa ajili ya Manunuzi ya Saruji Mifuko 3,000 lakini hadi wakati wa ufuatiliaji huu unafanyika tarehe 21/05/2018 mifuko ya saruji iliyopokelewa ilikuwa ni 600 tu kati ya 3,000 na hakukuwa na maelezo ya kuridhisha kutoka kwa wasimamizi kuhusu upungufu huo au kasoro hiyo. Aidha, katika mahojiano, Afisa Manunuzi wa Manispaa alikiri anakiri kufanyika kwa manunuzi hayo na kwamba ucheleweshaji huo umetokana na mzabuni huyo kuwa na mahitaji mengi ya wateja (order) na hivyo kushindwa kusambaza saruji kwa wakati. Matokeo ya ucheleweshaji huo ni kwamba saruji inayoendelea kutumika hadi sasa ni ile inayonunuliwa kutoka kwa wasambazaji wadogo wadogo mkoani Lindi ambao huuza kwa bei kubwa ikilinganisha na bei ya mzabuni.

ix. Ufuatiliaji ulibaini kuwa kampuni ya ulinzi ya 'Mwene Security' ilipewa kupewa kazi ya ulinzi na kuanza kupokea malipo kutoka kwenye fedha za mradi kiasi cha Tsh. 450,000/= kwa mwezi kuanzia mwezi Aprili 2018 bila ya kuwepo kwa kumbukumbu za tangazo, tathmini na

mkataba. Katika mahojiano na Kamati ya Usimamizi (KU) ya Kijiji walikiri kuwa kampuni hiyo ililetwa na viongozi wa ngazi ya manispaa bila ya wao kushirikishwa.

x. Ufuatiliaji ulibaini kuwa baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya havikuingizwa katika vitabu vya stoo (Store Legder) kinyume na K/F 59 cha Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2010 inayoelekeza bidhaa iliyonunuliwa kukaguliwa na mtaalamu na kuridhia ubora wake kabla ya kuingizwa katika kitabu cha stoo (store ledger). Mfano, ilibainika kuwa manunuzi ya nondo za 16mm, 12mm na 8mm kutoka kwa Mzabuni MURTUZA MOLEDNA MANJI ya Tsh. 11,133,040/= tarehe 20/04/2018 hayakuingizwa katika vitabu vya stoo vya mradi. Katika Mahojiano, Afisa manunuzi wa manispaa alionyesha stakabadhi za mzabuni na kueleza kwamba kwa bahati mbaya alisahau kuingiza taarifa hizo katika kitabu cha Stoo!

xi. Ufuatiliaji ulibaini kulikuwa na kupishana kwa 'ring beam' na kupinda kwa nguzo katika jengo la nyumba ya watumishi ambapo mhandisi msimamizi alililishuhudia tatizo hilo na kukubali kuwa fundi atapaswa kufanya marekebisho ya msingi kabla ya kuyapokea majengo hayo;

xii. Ufuatiliaji pia ulibaini kuwa zaidi ya asilimia 70 ya manunuzi yalikuwa yamefanyika bila ya kutolewa kwa stakabadhi za kielektroniki (EFDs). Hii ni kinyume na Kanuni namba 10(5) na 29(1) ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la thamani ya mwaka 2012.

### 10.3 Mapendekezo

Kufuatia matokeo ya ufuatiliaji huo, yafuatayo yalipendekezwa ili kuziba mianya ya rushwa kama ifuatavyo:

i. Afisa manunuzi wa Manispaa ahakikishe kuwa anasimamia ipasavyo sheria kanuni na taratibu za manunuzi ya umma katika ujenzi wa kituo cha afya cha Mnazi Mmoja mkoani Lindi

ii. Wajumbe wa Kamati ya Afya ya kata ya Mingoyo hawapaswi kufanya maamuzi ya kutumia fedha bila kuishirikisha kamati ya ujenzi ya kijiji hicho ili kukuza uwazi na uwajibikaji;

iii. Mhandisi Ujenzi wa Manispaa ametakiwa kupitia malipo yote ya mafundi na kufanya ukaguzi wa kazi walizofanya kabla ya kuzikubali/kuziidhinisha kwa malipo;

iv. Vifaa na bidhaa zote ziwekewe utaratibu wa kuingizwa kwenye ‘ledger store’ kama taratibu zinavyotaka
v. Elimu ya rushwa iendelee kutolewa hususani kwa wasimamizi wa miradi na viongozi wa halmashauri
vi. Mhandisi wa Manispaa anapaswa kuomba idhini kutoka kwa Katibu Mkuu-TAMISEMI kabla ya kubadilisha vipimo vya ujenzi kuwa tofauti na michoro na ‘BOQ’
vii. Manispaa iandae mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wasimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa utaratibu wa ‘force account’ bila kusahau mafunzo ya mara kwa mara ya manunuzi ya umma na usimamizi wa miradi (project supervision and management).

### 10.4 Mafaniko na Hitimisho

Lengo la ufuatiliaji huu lilikuwa ni kutathmini iwapo ujenzi wa kituo cha afya cha Mnazi Mmoja mkoani Lindi wanazingatia matumizi sahihi ya ‘force account’. Ufuatiliaji uliofanywa na ofisi ya TAKUKURU Lindi umebaini mianya ya rushwa ikiwemo ukiukwaji wa sheria ya manunuzi, kutowashirikisha wajumbe wa kamati za usimamizi na zile za afya, kufanya manunuzi ya vifaa na kutoorodhesha kwenye ‘store ledger’, kulipa mafundi bila taarifa ya ukaguzi, kufanya malipo bila kutoa risiti za EFDs, ucheleweshaji na ukiukwaji wa kifungu cha 59 cha Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa za mwaka 2010 inayoelekeza bidhaa iliyonunuliwa kukaguliwa kabla ya kupokelewa. Baada ya ufuatiliaji huo, matokeo yaliwasilishwa kwa uongozi wa manispaa ya wilaya ya Lindi na kujadiliana kwa pamoja namna ya kuzuia vitendo vya rushwa katika miradi ya ujenzi kwa kutumia utaratibu wa ‘force account’ ambao kwa siku za hivi karibuni umekuwa ukipigiwa kelele kuwa umegubikwa na vitendo vya wizi na rushwa. Uongozi wa manispaa walikiri kuwa utaratibu huu pamoja na faida zake unazo changamoto za kiutawala (governance challenges) ambazo hazina budi kutafutiwa ufumbuzi wa haraka. Mfano, Mhandisi wa Manispaa amekiri kuwepo kwa dosari/udhaifu katika ujenzi wa kituo cha afya cha Mnazi mmoja na kumwelekeza fundi mkuu kuhakikisha kuwa anafanya marekebisho ya msingi kabla ya kuukabidhi mradi na kulipwa fedha zake zote. Taasisi ilifanya ufuatiliaji ili kufahamu endapo udhaifu huo umerekebishwa na kubaini kuwa mkandarasi aliitikia agizo la uongozi wa manispaa

kwa kurekebisha sehemu zenye kasoro. Mradi uko katika hatua nzuri na endapo hakutojitokeza tatizo la fedha/usimamizi, mradi huo unatarajiwa kukamilika hivi karibuni. Pia uongozi wa manispaa ukiwakilishwa na Mhandisi wa Manispaa (Municipal Engineer) umeahidi kuzifanyia kazi dosari zote zilizoainishwa na ufuatiliaji wa TAKUKURU. Vilevile uongozi wa manispaa pia umeahidi kuendelea kuwaelimisha watumishi wake kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano za kupambana na rushwa kwa kufanya kazi kwa uadilifu, uaminifu na kujituma.

## 11.0 MIANYA YA RUSHWA KATIKA UNUNUZI NA USAFIRISHAJI WA ZAO LA UFUTA KATIKA WILAYA YA NACHINGWEA

### 11.1 Utangulizi

Kwa sasa kilimo kimekuwa siyo tu kwa ajili ya kujikimu, bali kimekuwa ni mfumo wa biashara ambao watu wanategemea kujikwamua kiuchumi. Kwa kadri mifumo ya maisha inavyobadilika, kukosekana kwa ajira na hata kutoridhishwa na kipato kisichokidhi haja kwa wale walioajiriwa; watu wengi sasa wanalazimika kujiingiza katika shughuli za kilimo ili kujiongezea kipato Kimsingi kilimo kimeonesha dalili nzuri za kuweza kumtoa mtu yeyote katika hali ya umaskini na kuwa katika hali nzuri ya kiuchumi ilimradi tu analima kitaalamu na kuwa mbunifu.Hii ni kwa sababu bado uhitaji wa mazao ya kilimo ni mkubwa ndani na nje ya nchi. Lakini pamoja na uwezo huu wa kilimo kubadilisha maisha ya watu wengi kiuchumi na kijamii nchini, bado kilimo chetu kina changamoto nyingi. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa mashamba bora, upatikanaji wa maji ya umwagiliaji kwa sababu mvua sio za uhakika na upatikanaji wa mbolea na mbegu bora. Mkulima mmoja mmoja hawezi kuzitatua changamoto hizi peke yake na kwa sababu hiyo analazimika kuwatafuta watu wengine wenye mawazo kama yake kuweza kuyafikia malengo wanayojiwekea. Kimsingi huu ndio ulikuwa mwanzo wa kuanzishwa kwa vyama vya msingi vya ushirika nchini mwetu.

Hata hivyo, pamoja na umuhimu wake, bado vyama vingi vya msingi vya ushirika vilivyopo katika wilaya ya Nachingwea havina uwezo wa kiuchumi wa kununua na kusafirisha wa baadhi ya mazao ikiwemo zao la ufuta. Hali ni mbaya zaidi katika mfumo wa ununuzi na usafirishaji wa zao hilo la ufuta.kwani baadhi ya vyama vya msingi vimegeuka kuwa mawakala wa walanguzi na kuacha jukumu lake la msingi la kuendesha biashara ya kununua na kuuza mazao ya wanachama wao kupitia vyama vyao na kuwa na sauti ya pamoja katika kutetea maslahi ya wakulima. Kutokana na hali hiyo, TAKUKURU Nachingwea ilifanya uchambuzi wa mfumo katika eneo hili kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika mfumo wa ununuzi na usafirishaji wa zao la ufuta ndani ya wilaya na kupendekeza namna bora ya kuziba mianya hiyo.

### 11.2 Matokeo ya Uchambuzi

i. Uchambuzi ulibaini kuwa taarifa za mapato ya ushuru wa zao la ufuta na mazao mengine hazibandikwi kwenye mbao za matangazo ya vijiji hali inayoashiria kutokuwepo kwa uwazi katika taarifa za mapato ya ushuru wa mazao na hivyo kuwapa mwanya viongozi wa vijiji kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu mapato ya ushuru wa mazao na kuyatumia mapato hayo kwa manufaa yao binafsi;
ii. Uchambuzi ulibaini kuwa vitabu na kumbukumbu za malipo ya ushuru wa zao la ufuta hazitunzwi vizuri katika vijiji vilivyofanyiwa uchambuzi;
iii. Uchambuzi ulibaini kuwa hakuna mfumo rasmi wa ununuzi wa zao la ufuta na hivyo kutoa mwanya kwa wafanyabiashara kununua zao hilo kiholela na kwa vipimo vinavyowapunja wakulima
iv. Uchambuzi ulibaini kuwa zao la ufuta katika wilaya hii linanunuliwa bila ya kuwa na kiwango maalumu kilichopangwa kwa ununuzi wa zao hilo kwa kila msimu wa mavuno;
v. Uchambuzi ulibaini kuwa kuna baadhi ya watendaji wa vijiji wamekuwa hawatoi stakabadhi za malipo ya ushuru kwa wafanyabishara wanaolipa ushuru wa mazao ikiwemo ushuru wa zao la ufuta;
vi. Uchambuzi ulibaini kuwa usafirishaji wa zao la ufuta hufanyika usiku baada ya kununuliwa katika vijiji vinavyozalisha zao hilo na hupitishwa kwenye vizuizi vya mazao vilivyowekwa katika halmashauri hiyo kwa njia ya rushwa;
vii. Uchambuzi ulibaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara wa zao la ufuta hutoa taarifa za uongo kwa viongozi wa kijiji na halmashauri kuhusu kiasi halisi cha tani/gunia kwa kupunguza idadi ya tani/magunia kwa lengo la kukwepa ushuru wa mazao.

### 11.3 Mapendekezo

Kufuatia matokeo ya uchambuzi huo, yafuatayo yalipendekezwa ili kuziba mianya ya rushwa

i. Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri (W) atoe agizo kwa watendaji wa vijiji kuweka taarifa za mapato na matumizi katika mbao za matangazo zilizoko katika ofisi za vijiji au sehemu nyingine ya wazi ili wananchi waweze kufahamu kiwango cha mapato na matumizi;

ii. Viongozi wa vijiji wanatakiwa kutunza vizuri nyaraka za ushuru wa mazao na nyaraka muhimu za kijiji kwa ajili ya kumbukumbu;

iii. Mkurugenzi wa Halmashauri na viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika katika wilaya hawana budi kuangalia namna bora ya ununuzi na usafirishaji wa zao la korosho kwa lengo la kuweka mfumo mzuri utakaompatia faida mkulima;

iv. Mkurugenzi mtendaji kupitia ofisi ya kilimo na ushirika kuhakikisha kuwa anapata bei elekezi ya ufuta na mazao mengine kutoka wizarani na kuwajulisha wakulima mapema iwezekanavyo;

v. Mkurugenzi mtendaji kupitia ofisi ya mweka hazina wa halmashauri apeleka stakabadhi za malipo zinazotumiwa na halmashauri katika ukusanyaji wa mapato katika vijiji vyote na kuwataka watendaji wote kutoa stababadhi hizo kwa wafanyabishara na wananchi wote wanapofanya malipo;

vi. Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri apige marufuku tabia ya kusafirishwa mazao nyakati za usiku ikiwemo kuchukua hatua za kinidhamu watumishi walioko katika vizuizi ambao wanaojihusisha na upokeaji wa hongo/rushwa;

vii. Kuimarisha usimamizi wa vyama vya msingi vya ushirika wilayani humo na kuahkikisha kuwa wakulima hawadhulumiwi na wafanyabiashara wenye tama ya kupata utajiri wa haraka;

viii. Elimu kuhusu rushwa iendelee kutolewa kwa viongozi na wananchi (wakulima)

### 11.4 Mafanikio na Hitimisho

Kuwekwa mfumo rasmi wa ununuzi na usafirishaji wa zao la ufuta katika vijiji vilivyoko ndani ya wilaya ya Nachingwea ni muhimu sana ili kulifanya zao la ufuta kuwa miongoni mwa mazao makuu ya biashara yanayowainua wakulima kiuchumi. Lengo la uchambuzi huu lilikuwa ni kufanya uchambuzi wa mfumo wa ununuzi na usafirishaji ili kubaini iwapo kuna mianya ya rushwa na kupendekeza namna ya kuiziba mianya. TAKUKURU ilibaini kutokuwepo kwa uwazi wa mapato na matumizi, kutokuwepo kwa mfumo wa kutunza taarifa za chama, kutokwepo kwa bei rasmi ya mazao na kusababisha uholela, kutokuwepo kwa bei elekezi ya ufuta na mazao mengine, watendaji kutotoa stakabadhi kwa wananchi wanpofanya malipo na tabia ya kusafirisha mazao nyakati za usiku na kutengeneza mazingira ya kuomba kupewa 'chochote'. Baada ya uchambuzi huu, matokeo yaliwasilishwa kwa wadau wa zao la ufuta na uongozi wa chama cha msingi cha ushirika cha wilaya ya Nachingwea umeahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa na Taasisi ili kuziba mianya ya rushwa. Pia uongozi umeahidi kuendelea kuwaelimisha wanachama na viongozi wake wote, na wale watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa watachukuliwa hatua kali za kisheria na kiutawala.

# Kwa Mawasiliano zaidi:

*Mkurugenzi Mkuu, Mtaa wa Jamhuri,*

*S.L.P 1291, 41101DODOMA.*

***Simu Nambari**: (026)2323315*

***Nukushi**:  (026) 2323332*

***Simu ya Bure**: 113*

***Barua Pepe**: dgeneral@pccb.go.tz*

***Tovuti**: www.pccb.go.tz*

***instagram**: takukuru.tz, **Facebook**: TakukuruTz, **Twitter**:TAKUKURU.TZ,*

***Online TV**: TAKUKURUTV*